Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 181 | JUMD.2 - SHA'BAN 1436 AH | APRIL/MAY 2015 | SHAH./HIJR. 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri -
Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.
Hiyo ni fadhili ya Mwenyezi Mungu Atampa Amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhili kuu. (62:3-5).

Khalifa Mtukufu awajibu wapinzani:

Hakuna nguvu iwezayo kuifuta Ahmadiyya juu ya uso wa ardhi

Na mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Kufuatia maamuzi ya kidhalimu ya Serikali ya Punjab nchini Pakistan kupiga marufuku maandishi kadhaa ya Jamaat, Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a kwenye hotuba ya sala ya Ijumaa ya tarehe 15/05/2015, alilizungumzia jambo hilo. Katika hotuba yake hiyo alisema:

Serikali ya Punjab huko Pakistan hivi karibuni imepiga marufuku uoneshaji hadharani wa baadhi ya maandiko ya Jamaat. Kwa msaada wa matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na utumaji wa ujumbe habari hizi zimeenea haraka sana duniani kote. Wanajumuiya wa Pakistan wamemuandikia Huzur kuonesha mashaka yao juu ya jambo hilo. Ni vyema ikumbukwe kwamba upinzani huu dhidi ya Jamaat si jambo jipya. Katika kipindi chote cha historia ya Jamaat, wale wajiitao viongozi wa dini wameendelea kuleta upinzani na kuweka ugumu juu ya Jamaat na hawatosita kufanya hivyo siku zijazo. Lakini mipango yao miovu haijawahipo kuidhuru Jumuiya siku za nyuma na kamwe haitoidhuru siku zijazo. Hadi sasa hakuna mama aliyekwishajifungua mtoto ambaye atakuja kusitisha ujumbe huu wa kimbingu wa Masihi Aliyeahidiwa a.s..

Chuki na Upinzani wao umezalika kutokana na choyo walichonacho juu ya maendeleo ya Jamaat na kiwango cha chuki walichanocho ni kikubwa kiasi hiki kwamba kinawafanya wapoteze mizania. Kinachojionesha ni hiki kwamba wale walio wasomi miongoni mwao ndio wabaya zaidi, na hawafanyi juhudi yoyote ya kupitia maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili kwamba wajionee utukufu na uzuri ambao Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika juu ya Mtume Muhammad s.a.w. na juu ya Islam. Watu wenye mawazo yasiyo na upendeleo wanashangaa wanaposoma maandiko yetu pale wanapojionea wenyewe ni kwa kiasi gani maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yanavyopotoshwa

Endelea uk. 2

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w: Mfano uliokamilika kwa wanadamu

Imefasiriwa na Dawati la Kiswahili, Morogoro

Inaendelea kutoka toleo lililopita

(Ilitolewa na Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, Khalifatul Masih II r.a. 26 Nov. 1933 wakati wa Jalsa ya Siratun Nabiyyi huko Qadian)

Baada ya kusoma Tashah hud, Ta'awwudh na Sura Fatiha Huzur r.a., alisema:

ULEZI WA BAADA YA KUFA

Kisha mwanadamu hufariki. Hata wakati huo pia ameuzingatia na kufahamisha kuwa ni namna gani maiti atendewe. Yeye alikuwa akiwaheshimu maiti wa kila kaumu. Wakati fulani maiti fulani ilikuwa ikipitishwa, basi akasimama katika kuiheshimu. Mtu fulani akamwambia ewe Mtume wa Allah, huyo ni Myahudi! Naye akamwambia kwamba hata Myahudi pia ni mja wa Mwenyezi Mungu. (Bukhari Kitabul Janaaiz, Babu man qaama bijanaazati yahuudiyyin). Kisha akasema muwataje kwa wema wale waliokwisha fariki. (Abu Daud Kitabul Adab, Babu fin nahyi 'an sabil mautaa).

Na yaweza kusemwa kwamba Mtume s.a.w. alikuwa akienda kuwapa pole wafiwa wa kila aliyefariki na kwa namna hii akawa pia amewafanyia malezi na akawa ametoa maagizo yote ya muhimu kuanzia kuzaliwa kwa mwanadamu hadi kifo chake. Na pia kama watu wote wachukuliwe mmoja mmoja, basi humo pia mtaonekana ulezi wake.

ULEZI WA KIROHO

Jambo kubwa kabisa kuliko yote ni hili kwamba yeye alikuwa ni mhimili wa maisha ya Akhera ya wote. Aliwaita watu wa kila kaumu washiriki ndani ya njia ya Mwenyezi Mungu. Alisema kwamba manabii wote walitumwa kwa watu wao lakini mimi nimetumwa kwa kaumu zote. (Bukhari Kitabus swalaat, babu qawlin Nabiyyi s.a.w. Ju'ilat liyal ardhu Masjidan wa twahuura). Sio hivi kwamba Islam imwambie mtu kwamba wewe ni mhindu, una uhusiano gani na mafundisho ya kiarabu. Bali yeye alileta ile nuru ambayo kwayo Allah Alisema: Laa sharqiyyatin wa laa gharbiyyatin (Sura An Nur: 36), isiyokuwa na uhusiano wowote na mashariki wala magharibi. Kwa namna hii akawa amethibitisha kuwa yeye ni mdhihirisho wa Mola wa walimwengu wote.

Mwanamke fulani alikuja kwa Hadhrat Isa a.s. na kumwambia nifundishe elimu yako. Lakini kwa kuwa mafundisho yake yalikuwa ni kwa ajili ya tabaka fulani tu la watu na mwanamke yule alikuwa hatokani na wigo huo, ndio sababu akamjibu hivi kwamba mimi siwezi kuziweka lulu zangu mbele ya nguruwe. (Mathayo 7:6) na siwezi kuwanyang'anya watoto chakula chao na kuwapa mbwa (Mathayo 15:26) na kwa namna hii akawa amemuambia kwamba mafundisho yangu yana mipaka. Lakini Mtume s.a.w. aliyaweka mafundisho yake kwa ajili ya viumbe wote na kwa namna hii akawa amekuwa mdhihirisho kamili wa Mola wa walimwengu.

ULEZI WA WOTE

Kwa uchache hali zote mbili za ulezi wa kimwili na kiroho utazikuta kwa wote. Riba imekatazwa kwa Wayahudi lakini pamoja na hayo wanaichukua kutoka kwa wengine (Kumbukumbu la Torati 23:19-20). Yeye s.a.w. alikataza riba, lakini kwa wote. Aliagiza kwamba kama kuna masikini yeyote mwenye shida, basi kuchukua riba toka kwake ni dhulma, kana kwamba hakubagua hata katika njia ya kimwili. Ingawa yasikitisha kwamba miongoni mwa Waislamu wameibuka watu wa aina hii ambao hufahamu kuwa inajuzu kuwalaghai wengine. Baadhi ya Masheikh wametoa fatwa kwamba inajuzu kuchukua riba kutoka kwa makafiri, ilhali kama kuna mtu yeyote anayehitaji kuhurumiwa, basi hata kama atokane na kaumu yoyote ile, anastahili kuhurumiwa. Na kama udanganyifu na ulaghai ni kitu kibaya basi kiwe kwa wote sio ifahamike kuwa ni kizuri kwa wengine.

Hadhrat Khalifatul Masih 1 r.a. alikuwa akisimulia kwamba mimi nilimpatia mtu fulani senti 50 kwamba alete kitu cha senti 25. Baada ya muda mchache akakileta kitu hicho lakini pamoja nacho akawa pia ameileta ile senti 50 na kusema kuwa leo nimemdanganya kafiri kweli kweli, nimechukua toka kwake fedha ya senti 25 na pia kitu cha senti 25. Kisha nikamwambia kuwa je una kitu

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KIWANDA CHA UKAFIRI

Kwa bahati mbaya sana kiwanda kinachotengeneza makafiri kinaonesha dalili zote za kupanuka siku hadi siku. Uwezo wake wa kufyatua makafiri umekuwa kiasi hiki ya kwamba ni wachache ambao hawakutengenezwa na kiwanda hiki cha fitina na hatari kubwa kwa mustakabali wa Islam. Chuki na uhasama mkubwa umejengeka kiasi hiki ya kwamba nduguyo wa kiroho anaonekana kinyaa na asiyefaa.

Yote hayo yanafanyika huku sote tukifahamu ya kwamba Qur'an Tukufu imesisitiza ya kwamba; 'Msiitane kwa majina mabaya' na kwa upande mwingine Mtukufu Mtume Muhammad (saw) anasema; "Anayemuita mwingine kafiri, yeye anakuwa kafiri". Ni jambo la kusikitisha mno kwamba historia ya Islam imejaa watu ambao walipewa lakabu ya 'kafiri' na lakabu hizi walipewa bila watowaji kufanya utafiti wa aina yoyote. Walisukumwa na husuda na roho mbaya.

Sir Seyid Ahmad Khan mwanzilishi wa vyuo vingi nchini India msomi wa hali ya juu na aliyewahamasisha Waislam watafute elimu ya kimagharibi, huyu naye hakupona aliitwa kafiri. Baba wa taifa la Pakistan Qaidal Azam Muhammad Ali Jinah aliyepata mahangaiko makubwa sana ya kutetea uhuru wa Waislam wa Pakistan na ambaye alikuwa anakasirishwa mara kwa mara na misimamo ya kuyumba ya Waislam hatimaye likazaliwa taifa la Pakistan; shughuli yote hiyo aliyoifanya haikuheshimiwa hata kidogo, naye aliitwa kafiri.

Yule Mshairi maarufu wa Pakistan na msomi wa hali ya juu Alama Muhammad Iqbal ambaye anaaminika ya kwamba ni mshairi bora wa Kiislam katika karne ya ishirini (20) alitukanwa sana, akadhalilishwa sana na kuambiwa ya kwamba hakuwa anajua chochote kuhusu Islam na hivyo hakuwa na sifa yoyote ile isipokuwa ni kafiri.

Kama ilivyo vigumu kwa tembo kupita kwenye tundu la sindano, hivyo inaonesha pia ni vigumu sawa na fat'wa ya Maulamaa wetu kumpata Muislam ambaye hawezi kupakwa tope hizi za ukafiri.

Lakini hii ina mustakbali gani kwa dini tukufu ya Islam? Uko wapi ule undugu na mapenzi yaliyokuwepo baina ya Waislam waliyopendana wao kwa wao na kuhurumiana? Wako wapi Waislam wanaoweza kuzima taa ili wageni wale na wenyeji wajifanye kwamba wanakula? Wako wapi Waislam wale ambao katika vita kila mmoja alimpendelea mwenzie wa Kiislam aanze kunywa maji kabla yake na hatimae wote wakafa bila kuyanywa maji hayo. Wako wapi Waislam ambao wanaamini ya kwamba Waislam ni sawa na mwili mmoja na sehemu yoyote ya mwili ikiwa inaumwa mwili hauwezi kuwa vizuri?

Lakini inabidi tukumbuke Bwana wetu mpendwa, Kiongozi wetu, chem chem ya rehema zote, yeye alitumwa kuwa rehema kwa viumbe wote aliwahurumia viumbe wote, hata kinda wa ndege aliamuru waachiliwe huru. Matendo yetu ya leo ya kutesa, uhasama n.k tunawezaje kujiita sisi ni wafuasi wake? Inasikitisha mno ya kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliendelea kulia kwa ajili ya maendeleo ya Islam, kwa ajili ya Amani duniani. Tunatakiwa tuheshimu na kuthamini juhudi hizo. Na njia ya kuenzi hayo ni kukumbuka daima kuwa kila nukta ya maisha yetu fikra zetu, kufanya kazi kwetu, kutembea, kula, kulala, tufuate mfano unaong'ara wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hiyo tu ndiyo dawa mujarabu ya kutatua matatizo yanayomkabili binadamu kwa hivi sasa.

Wasiwasi wetu mwingine ni kwamba kiwanda cha kuchafuana, matusi, kashfa nacho taratibu kinaanza kazi kutokana na upepo wa kisiasa unaovuma nchini. Ni kweli ya kwamba kila mtu ana haki ya kutoa maoni yake, lakini bila shaka kumuumiza mwingine kwa njia yoyote ile hauwezi kuwa ni utamaduni wa nchi hii. Tumezoea utamaduni wa kuheshimiana na kusikilizana. Wakati huu kuliko wakati wowote ule tunaomba uvumilivu na uteuzi wa maneno wakati huu nyeti ambapo kila mtu anatumia haki yake ya Kidemokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa. La msingi katika harakati zote hizi tukumbuke ya kwamba sisi ni Watanzania. Na Tanzania ina utamaduni na silka yake. Kinachotakiwa ni ujengaji madhubuti wa hoja, na wala sio hoja ya nguvu. Ni vizuri basi tukakumbuka maneno ya Mshairi Sheikh Kaluta Amri Abedi aliyeimba;

"Nakuasa usikie, usemaji ni karama
Maneno usirukie, sema mambo kwa kupima
Utamkapo ujue, neno halirudi nyuma
Ukosapo neno jema, heri kujinyamazia".

Khalifa Mtukufu awajibu wapinzani

Kutoka uk. 1

na kuzuliwa uongo na wapinzani wetu. Watu hawa huonyesha kustaajabishwa kwao kupitia vipindi vya moja kwa moja vya MTA na pia huwa wanamuandikia Huzur wakieleza kwamba sasa wametambua adhama ya maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambapo viongozi wao wa dini walikuwa wakiwashindilia kubaki ujingani.

Wapinzani wetu wanaweza kufanya vyovyote wapendavyo lakini njama zao hazitotudhuru chochote zaidi ya kuamsha imani zaidi ndani yetu na kukuza maungano yetu na Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Achilia mbali serikali ya Panjabi hata kama dunia yote iungane katika juhudi za kutuwekea vipingamizi, kazi yetu haiwezi kusimama kwa sababu ni kazi ya kimbingu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu amemtuma Masihi Aliyeahidiwa a.s. na amempatia hazina za kiroho na akamuahidi ushindi pia. Kwa kadri wapinzani wetu watakavyoongeza kutupinga, ndivyo pia yatakavyokuwa makubwa maendeleo yetu, Inshallah. Mambo yataendeleo kuwa hivyo siku zote.

Hivyo hakuna sababu yoyote ya kuwa na hofu kwani sasa vitabu vyetu vinachapwa katika nchi mbalimbali duniani. Vitabu vyetu vinapatikana kwenye mtandao na pia vipo kwenye mfumo wa sauti. Zilipita zama ambapo vikwazo vya kuchapisha vitabu vyetu vingeweza kuleta hofu lakini sasa hazina za elimu ya kiroho zimesambaa duniani kote na ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunajipatia faida ya hazina hizo kwa kiwango cha juu.

Hivyo basi Huzur akasema: Anaamua (na kuagiza kwamba) kuanzia sasa darsa za vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. zitiliwe mkazo zaidi kuliko hapo kabla; ili iwe hivi kwamba vikwazo vilivyowekwa katika jimbo moja la Pakistan, vibadilike kuwa faida kwa kila mmoja wetu.

Darsa hizo zitatolewa kwa lugha ya asili ambayo kitabu fulani kiliandikwa, lakini tafsiri yake itapatikana kwa lugha kadhaa. Wale waliojenga hofu juu ya hali hiyo wazitupilie mbali hofu zao hizo. Vikwazo hivyo kwa mara nyingine vinaweka wazi nukta hii: Watu hawa wanadai kuwa na mapenzi makubwa ya Mtume Muhammad s.a.w. na hudai kwamba upinzani wao juu yetu umezalika kutokana na mapenzi makubwa waliyonayo juu ya Mtume Muhammad s.a.w. (wakidai kwamba vitabu vyetu vinamdhalilisha Mtume Muhammad s.a.w.) lakini hawajawahipo hata siku moja kusoma maandishi yetu kwa njia isiyo ya upendeleo.

Basi hotuba ya leo itaangazia kwenye baadhi ya maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. (aliyoandika juu ya Mtume Muhammad s.a.w.) - Maandishi ambayo wapinzani wetu wanadai kwamba yanashusha heshima na adhama ya Mtume Muhammad s.a.w.. Linakuwa ni jambo la kushangaza kwa mtu yeyote anayedai kumpenda Mtume Muhammad s.a.w. na kisha moyo wake usiguswe na chochote na kujaribu kuyaelewa zaidi (maandishi yetu) hata baada ya kuyasoma au kuyasikia.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika:

Mpango wa Mwenyezi Mungu kuhusiana na Mitume na Mawalii (marafiki wa Mwenyezi Mungu/watawa/watu watukufu) ni huu kwamba kila aina ya khulka yao njema ni lazima idhihirishwe na kwa uwazi kabisa ithibitishwe. Kwa kutimiza mpango huu Mwenyezi Mungu huyagawanya maisha yao matakatifu kwenye sehemu kuu mbili. Sehemu moja huwa wanapita kwenye shida na matatizo makubwa ambamo huteswa na kuhangaishwa sana kwa kila hali, ili kwamba zile khulka zao njema zidhihirike ambapo zisingeweza kudhihirika bila ya kupitia kwenye ugumu mkubwa. Iwapo wasingeingizwa kwenye shida kubwa, ingewezaje tena kusemwa kwamba hawa ni watu ambao hawamuasi Mola wao hata katika shida kubwa kiasi gani, bali kinyume chake daima wanaendelea kusonga mbele (kwenye kumcha Mola wao).

Daima wanakuwa wenye shukurani juu ya fadhila za Mwenyezi Mungu kwa kuwateuwa kwao kuwa dhihirisho la rehema Zake na wanajihesabu kuwa na bahati njema (thamani) kwa kuteseka katika njia yake Mwenyezi Mungu. Hivyo Mwenyezi Mungu anawapitisha kwenye matatizo na shida ili kudhihirisha subira yao, uimara wao, ujasiri wao, uvumilivu wao, utii wao na ushujaa wao mbele ya dunia - kwa njia hiyo hudhihirisha ndani yao ule usemi kwamba (Uimara ni jambo kubwa zaidi kuliko muujiza), kwa sababu uimara uliokamilika hauwezi kubainika iwapo hapana shida na mashaka makubwa, na pia kiwango cha juu cha uvumilivu na subira navyo haviwezi kudhihirishwa isipokuwa kwenye mazingira ya majaribio makuu.

Majanga haya kwa hakika ni mbolea (baraka) kubwa kwa Mitume na Mawalii ambapo kupitia hayo tabia zao za hali ya juu ambazo ni za kipekee na hazina mfano wake zinapata kudhihirika na vyeo vyao vinaongezeka zaidi kwenye maisha yajayo. Iwapo wasingepambana na shida hizi, wasingeweza pia kufikia baraka hizi, na pia sifa zao zenye kushangaza zisingeweza kubainika mbele ya watu wa kawaida, na hivyo wangeliwachukulia kuwa kama watu wengine tu na wako sawa na wao.

Kwani hata kama wangeishi maisha yao haya mafupi kwa raha na starehe, bado lazima ilikuwa siku moja waagane na maisha haya yasiyo ya kudumu. Kwa hali hiyo raha na starehe zao hazingeweza kubaki nao daima, lakini pia wasingeweza kupata madaraja ya juu huko Akhera, bali pia ujanadume wao, umahiri wao, umakini wao na ujasiri wao usingekubalika kiujumla, sifa ambazo zinawathibitisha kutokuwa kwao na mfano, kutokuwa kwao na rika, kuwa wenye upekee wa aina yao, uliojificha zaidi ya kujificha kwa namna ambayo hakuna anayeweza kuuwazia, na pia ni wakamilifu kwenye ujasiri kiasi hiki kwamba kila mmoja wao alikuwa ni kama simba elfu moja kwenye mwili mmoja na kama duma (chui) elfu moja kwenye sura moja, ambao nguvu yao inazidi tafakuri ya mtu yeyote na ilifikia ukaribu wa ndani sana na Mwenyezi Mungu.

Sehemu ya pili ya maisha ya Manabii na Mawalii ni ile ambayo hupata madaraja ya juu ya ushindi, heshima na utajiri, ili kwamba waweze pia kuonesha zile sifa zao tukufu ambazo zinaweza tu kuoneshwa na yule mtu aliyepata ushindi, heshima, utajiri, mamlaka, utawala na nguvu.

Kumiliki utajiri na nguvu ni masharti ya lazima ili kuthibitisha kwamba mtu

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Khalifa Mtukufu awajibu wapinzani

Kutoka uk. 2

anazo sifa (khulka njema) za kuwasamehe waliomtesa, kutokuwalipiza kisasi wale waliomdhulumu, kuwapenda maadui zake, kuwatakia mema wale wasiomtakia chochote isipokuwa ubaya, kutokupenda utajiri, kutokujiwachia kufanya kiburi kwa sababu ya utajiri wake lakini pia kutokufanya ubahili na kuukunja mkono wake, kuwa mkarimu na mwenye kutoa sana, kutokutumia mali kutimiza matakwa ya kimwili tu na kutokutumia mamlaka na uongozi kama silaha ya ukandamizaji na kuchupa mipaka.

Sifa hizi zinawezekana tu kudhirika iwapo mtu amefikia vyote viwili utajiri na mamlaka. Bila ya kupitia vipindi vya majaribu na bahati mbaya, na pia vipindi vya mafanikio na mamlaka, makundi haya mawili ya khulka njema hayawezi kudhihirishwa. Hii ndio sababu hekima kamilifu ya Mwenyezi Mungu ikapenda kwamba mitume na mawalii wapatiwe aina zote mbili za mazingira ambazo ndani yake kuna maelfu ya baraka.

Utokeaji wa hali hizi mbili ingawaje, hazifuati mpangilio mmoja kwa wote. Hekima ya kiungu huamua kwamba kwa baadhi yao kipindi cha amani na raha kije kwanza na kisha ndipo kifate kipindi kigumu cha mashaka; wakati ambapo maisha ya wengine huanza na mawimbi magumu na nusra ya Mwenyezi Mungu hufata mwishoni.

Katika maisha ya baadhi yao vipindi hivyo viwili huambatana na havijitofautishi bayana.

Katika hali zote hizi, Hadhrat Khaatamur-Rusul (Muhuri wa Manabii) s.a.w alizipitia kwa ukamilifu wake na kwa namna ambayo khulka zote tukufu za Mtume Muhammad s.a.w. zilidhihirika mithili ya jua na hivyo maana ya 68:5 (Wainnaka Laalaa Khuluqin adhiim) ikadhihirika kwa ukamilifu wake.

Zaidi ya hayo, Mtume Muhammad s.a.w. akiwa amethibitika kuwa mkamilifu kwa aina zote za khulka, pia anasimama kama shahidi juu ya tabia zilizotukuka za manabii wote, kwa sababu ameuthibitisha ukweli wa manabii wote, amevisadikisha vitabu vyao na ameionesha dunia kwamba kwa hakika manabii wote walikuwa ni wateule wa Mungu.

Upembuzi huu pia unafukuzilia mbali hisia zinazoweza kuzuka kumhusu Masihi Yesu kwamba khulka njema za Hadhrat Isa bin Mariam a.s haziwezi kuthibitishwa kwa kiwango kilichokamilika katika aina zote mbili za makundi ya khulka njema yaliyotajwa juu, lakini pia kwamba eti haziwezi kuthibitishwa hata kwa aina moja kati ya aina hizo mbili.

Eti kwa sababu Yesu alionesha subira lakini katika hali ya kutingwa kabisa na kwamba ukamilifu wa sifa hiyo ungeweza kufikiwa tu kama Masihi mwana wa Mariam angeweza kupata mamlaka na nguvu dhidi ya watesi wake na kwamba angeliwasamehe kutoka kwenye moyo wake wale waliomtesa, kama vile alivyofanya Hadhrat Khaatama Nabiyyiin ambaye alipata ushindi kamili juu ya watu wa Makka na wenginewao na baada ya kufikia hali ambayo inaweza kusemwa kwa dhahiri upanga wake ulikuwa shingoni mwao, lakini akawasamehe makosa yao na akawaadhibu wale wachache tu ambao walifanya makosa ya jinai na kukawa na amri ya wazi ya Mwenyezi Mungu kwamba watu hao waadhibiwe Ukiondoa hao wachache ambao walihukumiwa kila adui wa hatari kabisa alisamehewa. Na akiwa amepata ushindi Mtume Muhammad s.a.w. alitangaza (hakuna lawama juu yenu leo). Kutokana na kusamehewa makosa yao - ambapo ilionekana ni jambo lisilowezekana kwa wapinzani wa Mtume Muhammad s.a.w., ambao waliyahesabu madhambi yao kuwa yaliwastahilia kifo mbele ya yule aliyewashinda - maelfu kati yao walijiunga na Islam mara moja. Hivyo uimara ulio mnyofu wa Mtume Muhammad s.a.w. ambao aliudhihirisha kwa kipindi kirefu chini ya mateso makali waliyomfanyia iling`aa mbele yao mithili ya jua.

Kama ambavyo ni sehemu ya tabia ya asili ya mwanadamu kwamba utukufu na ukuu wa subira unaweza kuoneshwa kwa ukamilifu na mtu yule tu ambaye baada ya kipindi cha kuteswa ameonesha msamaha, kwa waliomtesa na baada ya kupata nguvu za kuwaadhibu. Hii ndio sababu khulka za hali ya juu za Masihi kuhusiana na jambo la uvumilivu na upole na uvumilivu haukujionesha vya kutosha, na pia haikuwa wazi kwamba uvumilivu na upole aliokuwa nao ilikuwa ni wa hiyari yake au ulikuwa ni wa kulazimishwa. Kwa sababu Masihi hakuwahi kupata nguvu na mamlaka ili kwamba ikashuhudiwa kuwa angeliwasamehe maadui zake au angeliwalipiza kisasi.

Tofauti na hilo, khulka njema za Mtume Muhammad s.a.w. zilidhihirika na kupitishwa kwenye mtihani katika mamia ya matukio na ukweli wao ukang'aa mithili ya jua. Sifa zake nzuri za wema, moyo mkuu, ukarimu, kutokujipendelea, unyenyekevu, ushujaa, utawa, kutosheka na kujiepusha na starehe za kidunia zilidhihirika bayana na kwa uwazi sana kwa Mtume Muhammad s.a.w. kiasi hiki kwamba sio Masihi tu, bali hakuna nabii yeyote wa kabla yake aliyewahi kuzidhihirisha kwa kiwango alichozidhihirisha yeye.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu alifungua kwa ajili ya Mtume Muhammad s.a.w. milango isiyohesabika ya hazina za kidunia, alizitumia hizo zote katika njia ya Allah na hakutumia hata senti moja kwa njia ya kujifaidisha binafsi. Hakujenga majumba wala mahekalu, bali alitumia maisha yake yote akiishi kwenye kibanda cha tope ambacho hakikuwa na tofauti yoyote na vibanda vya maskini wengine. Alilipa uovu aliofanyiwa kwa wema na aliwasaidia waliomtesa kwa kuwatatulia shida zao kwa kutumia mali yake.

Kwa kawaida alikuwa akilala chini, akiishi kwenye kijumba kidogo na kwa kawaida alikuwa akijipatia mkate tu kwa ajili ya kula au wakati mwingine hakuwa na chochote cha kula. Huyu ni mtu ambaye aliruzukiwa utajiri mwingi wa kidunia, lakini hakuzamisha mikono yake kwenye utajiri huo bali daima alipendelea ufukara kuliko utajiri na alipendelea unyonge kuliko kuonekana mwenye nguvu. Kutoka siku aliyotangaza kutumwa na Mungu hadi siku aliyoaga na kwenda kwa Rafiki yake Mpendwa, hakuonesha na kukipa umuhimu kitu chochote zaidi ya kumuabudu Mungu Mwenye Enzi. Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu ndipo alidhihirisha ushahidi wa ujasiri wake, ukakamavu na uimara katikati ya mapigano akikabiliana na maelfu ya maadui na huku kifo kikionekana ni kitu kisichokwepeka.

Hivyo hivyo Mwenyezi Mungu alipelekea kwamba sifa zingine za kuwa na moyo mwema na mkuu, ukarimu, kutosheka, ushupavu, ushujaa na mapenzi kwa Mungu yajidhihirishe ndani ya dhati ya Hadrat Khatamul-Anbiya' kwa namna ambayo hayajawahipo kujidhihirisha kwa Nabii yeyote wa kabla yake na pia haitotokea kamwe baada yake.

Kwa upande wa Hadrat Masih a.s. khulka hizi njema hazikubainika bayana kwa sababu khulka hizo zinaweza kuthibitika tu pale mtu afikiapo pia kushika mamlaka na utajiri na Masihi hakuwahipo kushika mamlaka na utajiri. Kwa namna hii khulka zake njema zinabakia kuwa zimefichama kwa sababu mazingira ya kuzidhihirisha hayakutokea.

Ingawaje pingamizi hiyo iliyotajwa juu kumhusu Masihi imeweza kufutiliwa mbali na mfano uliotukuka wa Mtume Muhammad s.a.w., kwa namna ambayo mfano wake uliobarikiwa na uliokamilika umeziba mapungu yanayoweza kusemwa katika khula za kila nabii na kwa kupitia yeye chochote ambacho kilibakia kuwa kimefichama kwenye khulka za Masihi bali na manabii wengine wote kilijitokeza kwa mng'ao mkubwa.

Wahyi na Utume ulifikia kikomo ndani ya dhati yake kwa maana kwamba uzuri wote (unaoweza kudhirishwa na Manabii) ulifikia kilele kwake. Na hii ni fadhili ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye. (Barahin e Ahmadiyya, Part III, pp. 177 – 181)

Pia Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika:

Ninao uzoefu binafsi kwamba kumtii Mtume Muhammad s.a.w. kwa moyo wote na kumpenda kwa mapenzi ya kweli, hatimae humfanya mtu naye apendwe na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu huzalisha ndani ya moyo wa mtu huyo vuguvugu la mapenzi Yake, na kuundoa moyo wa mtu huyo kutoka katika kila kitu isipokuwa kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na ashiki na matamanio yake daima yanabaki kwa Mungu Mmoja Mwenye Enzi.

Na hapo ndipo onesho maalum la mapenzi ya Mungu linapomuangukia mtu huyo na kumpatia rangi kamili ya mapenzi ya kujitolea, na kumvuta kuelekea Kwake kwa mvuto wa nguvu. Na hapo ndipo anapopata nguvu ya kuyashinda matamanio yake na kutoka kila upande kazi zisizo za kawaida za Mwenyezi Mungu zinamjia kama ishara ya kumpa nguvu na kumsaidia. [Essence of Islam, Vol. I, p. 210 - Haqiqat-ul-Wahi, Ruhani Khaza'in, Vol. 22, pp. 67-68]

Pia ameandika yafuatayo kumhusu Mtume Muhammad s.a.w. :

Mtu ambaye ndani ya dhati yake na sifa zake na matendo yake na kwa vipaji vyake vya kiroho alionyesha mfano wa juu wa ukamilifu katika elimu na matendo mema na kuonyesha ikhlaswi na uimara mkubwa kiasi hiki kwamba akatajwa kuwa ni mtu mkamilifu alikuwa ni Muhammad s.a.w. ..... Mtu ambaye alikuwa ni mkamilifu kama mtu na kama mtume, na aliyekuja na baraka kamili, na ni mtu ambaye kwa kupitia uamsho na ufufuo wake wa kiroho alidhihirisha (kiama) hukumu cha kwanza duniani na kuwafufua wafu wa kiroho, mtume huyu aliyebarikiwa, Muhuri (Mbora) wa Manbii wote, kiongozi wa wachamungu wote, fahari ya Manabii ni Muhammad mteule s.a.w.. Mungu wetu alishusha duniani kupitia Mtume huyu baraka ambazo hajawahipo kuzishusha kwa yeyote tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

Lau kama mtume huyu mkuu asingelidhihiri duniani basi dunia isingekuwa na ushahidi wa ukweli wa nabii yeyote mdogo wa kabla yake kama vile Nabii Yunus, Yakub, Isa Mwana wa Mariam, Yahya, Zakaria n.k. (a.s.). Kwani ingawaje walibarikiwa na kutukuzwa na Mwenyezi Mungu na walikuwa ni wapenzi wa Mungu Mwenye Enzi, wanawiwa na Mtume huyu kwamba wamekubaliwa na wanadamu kwamba walikuwa manabii wakweli kupitia ushahidi wake. Ee Allah mshushie rehema Mtume huyu na pia uzishushe juu ya watu wake na masahaba zake wote. Na neno letu la mwisho ni hili: Kila sifa njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu wote.

[Essence of Islam, Vol. I, p. 199 - Itmam-ul-Hujjah, Ruhani Khaza'in, Vol. 8, p. 308]

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia ameandika:

Hapana Nabii yeyote aliye sawa na Mtume Muhammmad s.a.w. na hapana kitabu chochote kilicho sawa na Qur'an Tukufu chini ya mbingu. Na Mungu Hakupenda kwa yeyote awe mzima wa milele ila kwa Mtume huyu mtukufu aliye ni mzima wa milele. Yaani Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumuweka mzima wa milele amefungua chemchem ya sheria yake na baraka za utukufu wake kuendelea mpaka siku ya Kiama. Na mwisho kwa baraka ya utukufu wake amemtuma dunia Masihi Aliyeahididwa ambaye kuja kwake kulikuwa ni lazima kwa kukamilisha jengo la dini tukufu ya Kiislam. Maana ilikuwa lazima kwamba dunia hii isiishe mpaka aje Masihi mmoja aliye kwa asili ya roho mfano wa Nabii Isa, katika umati wa Muhamamd s.a.w. kama ulivyopewa umati wa Musa.

Na aya hii ya Quran: Ihdinaswiraatwal Mustaqiim siraatwaladhiina ana amta alaihim - utuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale uliowaneemesha, inadhihirisha jambo hili. Na Mussa s.a.w. alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa zamani na Mtume Muhammad s.a.w. alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa nabii Musa a.s. Na silsila ya Mtume Muhammad s.a.w. inaizidi silsila ya Musa a.s. kwa fadhila nyingi mara elfu nyingi zaidi. Na mfano wa Musa (Mtume Muhammad s.a.w.) ni bora kuliko Musa, na pia mfano wa Issa (Masihi Aliyeahidiwa a.s.) ni bora kuliko Issa a.s. (Kishti Nuh, Ruhani Khaza'in, Vol. 19, p. 14) (Kwenye Safina ya Nuhu kwa Kiswhaili uk. 10).

Mwisho

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ni mfano uliokamilika

Kutoka uk. 1

fulani? Hebu nionyeshe. Hicho kilikuwa ni kitu ambacho kwa kawaida mwenye duka hukiweka ndani. Yeye akaenda ndani kukichukua lakini akasahau kuiweka ile senti 25 ndani ya sanduku la fedha nami nikaichukua na kuiweka mfukoni. Hivyo baadhi ya Waislamu hufahamu hiyo kuwa yajuzu, lakini hayo si mafundisho ya Kiislamu hata kidogo. Mafundisho ya Kiislamu ni haya tu kwamba uwafanyie wote uadilifu na haki. Kusiwepo na ubaguzi huu katika masuala ya kidunia.

KUKATAZWA KWA UBAGUZI WA RANGI NA WA KIKABILA

Mbali na hiyo, yeye aliufuta ubaguzi wa rangi na wa kikabila. Ndani ya Makanisa ya Wakristo, viti vya matajiri na masikini vimetenganishwa. Kwa wahindu kuna wale walio achut (watu wa daraja duni) na walio Brahman (watu wa daraja lililotukuka), kwa wayahudi kuna bani Harun na wengine bani Lawi. Lakini yeye s.a.w. alisema ubaguzi wa kikabila si kitu chochote. Yeyote afanyae wema kati yenu ndiye aliye mkubwa. (Al Hujurat:14).
Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika ninyi.
Na yule aliye mtukutu, mwongo na mtenda maovu, awe wa namna yeyote ile ni mbaya. Madhumuni haya yameizunguka sehemu za dini zote lakini hapa zaweza tu kuashiriwa kwa kuwa wakati wa Magharibi umeshafika.

UFUNUO WA MWENYEZI MUNGU

Kisha sifa ya kiRahmani inakuja, maana yake ni hii kwamba, kwa kile kitu Alichokiumba ametoa pia nyenzo na njia ya kukitumia. Chini yake twaona kwamba; je kwa ajili ya hata kuiendesha kazi ya mtu asiyestahiki, (Mtume s.a.w.) alitengeneza nyenzo yoyote? au kabla ya kuanza kazi aliandaa mpango wowote wa kuiendesha? Katika hali hii jambo la kwanza linalostahili kukumbukwa ni hili, kwamba kile kitu kipatikanacho bila ya juhudi yoyote ni ilham. Katika zama zake mlango wa Ilhaam ulikuwa umefungwa na ilikuwa ikifahamika hivi kwamba sasa mlango wa ilham umefungwa na ilham ilikwisha malizikia kwa waliopita na kulikuwa hakuna tumaini lolote kwa vizazi vijavyo kuipata.

Yeye alizifikiria hisia za watu na akasema kwamba hata sasa mlango wa ilham uko wazi. Kama kwa mtu fulani kuna uwezo na asili ya kukipata kitu fulani, lakini yeye hana hata wazo kwamba mimi naweza kukipata kitu hiki, sasa yeye atafanya juhudi gani ya kukipata kitu hicho. Kama kuwe na hazina ndani ya nyumba ya mtu fulani lakini mwenyewe asiwe hata na habari sasa yeye atapata faida gani?
Hivyo nguvu zimo ndani ya wote na Mwenyezi Mungu Ameweka ndani ya kila ubongo uwezo wa kupata ilham. Lakini hiyo hupatikana kutokana na matumaini na kutawakali (kwa Mwenyezi Mungu) naye alijengesha matumaini yake duniani kote kwamba, hata sasa mlango wa ufunuo u wazi kwa ajili yake. Na yapaswa kukumbuka kwamba kwa ajili ya kupata ilhaam, mlango pekee ni wa matumaini na kutawakali. Mwenyezi Mungu Humtendea mja sawa na rai yake. Mtume s.a.w. alisema kwamba Mwenyezi Mungu Ameniambia: Anaa 'indad dhwanni 'abdii bii yaani Mimi Humtendea mja wangu jinsi anavyonidhania. (Bukhari Kitabu Tawhid Bab qawlil laahi taala yuriiduuna an yubaddiluu kalaamal Laahi).
Kama waseme kwamba mlango wa ufunuo umefungwa, basi Nami pia Nasema hivyo hivyo; sawa umefungwa. Na kama waseme kwamba lazima tutakutana na Mwenyezi Mungu, basi Nami pia Husema hivyo hivyo; safi kabisa njooni tukutane. Yeye aliingiza matumaini haya ya kiroho na akaufungua mlango wa kutawakali.

MPANGO KAMILI WA KUWASAIDIA MASIKINI

Hata kimwili ninatoa mfano wake mmoja. Dini zote zimetoa hukumu ya swadaka, lakini kama kazi hii haifanyiki chini ya nidhamu fulani basi haiwezi kukamilika. Kila mmoja atasema vizuri, tutatoa. Haifahamiki chochote kuhusiana na lini atatoa na nini atakachokitoa. Lakini Mtume s.a.w. alitoa kanuni fulani kuhusiana nayo kwamba kila mtu mwenye nguvu na uwezo analazimika kila mwaka kutoa kiasi fulani kilichokadiriwa kwa ajili ya wenye kuhitaji wasio kuwa na kazi, ambazo zitakusanywa sehemu moja na kugawanywa kwa wote wenye mahitaji. Kwa namna hii akawapandisha juu masikini na hii pia ni kazi iliyo chini ya sifa ya kiRahmaani. Wakati haupo waila kama ufafanuzi wake uelezwe basi itafahamika kwamba ni namna gani ameufunga mlango wa wizi, ujambazi na vurugu.

MDHIHIRISHO KAMILI WA SIFA ZA KIRAHIMI

Sifa ya tatu ni ya Rahim ambayo maana yake ni hiii kwamba malipo ya kazi kubwa kabisa ndiyo yatolewe. Watu wema daima huwa wakilipiana hisani, kwa mfano mtu fulani humwita mwingine akimsema Mheshimiwa, basi mtu huyo atasema tafadhali karibu mheshimiwa. Mmoja anasema wewe ni mtu mzuri sana, mwingine anasema, mimi ni nini bwana, siwezi hata kidogo kushindana nawe. Lakini ustaarabu huu uko kwenye mpaka huu kwamba haitamletea hasara, lakini ipatikanapo hasara binafsi basi husahau kila kitu. Watu wa Delhi wanaitwa Mirza sahib na watu wa Lucknow wanaitwa Mir sahib na wote hao ni mashuhuri katika ustaarabu na umaridadi.
Inasemwa kwamba wakati fulani Mir wa Lucknow na Mirza wa Delhi walikutana stesheni. Wote wawili wakaonelea kwamba ni bora wadhihirishe ustaarabu wao kwa uwazi kabisa, isije akafahamika na mwenziwe kuwa hajastaarabika, kwa hiyo Mir sahib akasimama mbele ya gari moshi na kusema huku akiinama: Mirza sahib, tafadhali safiri bwana na huku akiendelea kuinama (kwa heshima). Na Mir sahib naye akawa ameinama zaidi kuliko yeye akisema: Wewe tafadhali ndio utangulie, mimi niliye duni, sina haki ya kutangulia. Watu waliendelea kupakia mizigo ndani ya gari moshi na kuketi, lakini hawa wawili wakawa wamesimama mbele ya mlango wakionyesha ustaarabu wao. Lakini mara treni ilipopiga honi ya kuashiria kuondoka, basi mmoja wao akamsukuma mwenzake akisema: Ewe mwenye bahati mbaya, nipishe niingie ndani. Hivyo pale ipatikanapo fursa ya kufanya kurbani, basi ustaarabu wote huwa hauna tena umuhimu.

KUBEBA HASARA KWA AJILI YA WENGINE

Lakini Mtume s.a.w. baada ya kupata hasara alitoa badala yake ukarimu. Kila nabii alitoa bishara ya kumhusu na kusema kwamba atakuja mtu wa aina fulani na watu watafaidika naye. Idadi ya wale waliosilimu kutokana na bishara hizo ni ndogo sana ukilinganisha na wale waliosilimu baada ya kuyaona mafundisho ya Kiislamu. Wale watu ambao Mtume s.a.w. aliwavuta kutokana na mafundisho yake na khulka zake njema, idadi yao ni kubwa sana lakini hata hivyo aliwasaidia wengine kwa kujidhulumu mwenyewe. Kwa sababu kama jambo hili likubaliwe kwamba hata mitume wa hapo kabla nao pia walikuwa ni waongofu, basi ugomvi huu ungeweza kutokea kwamba sasa kulikuwa na haja gani ya yeye kuja. Na kama angesema hivi kwamba wale wote wa kabla ni wezi na wanyang'anyi na mimi ndiye nabii, kwani dunia ilikuwa ikihitaji kiongozi mwema, basi ingekuwa rahisi sana kwa ajili yake. Lakini haikuwa hivyo bali akasema kwa ajili ya kuilipa hisani hiyo;

Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji (35:45)
Huenda watu ishirini, au mia au mia mbili hivi walijiunga na Uislamu kutokana na bishara za mitume hao, lakini yeye aliwaaminisha utakatifu wao (Manabii waliopita) mamilioni ya watu na kwa namna hii kwa hisani hii ya kawaida tu akawa ametoa malipizo yenye shani ya juu kiasi gani na alitoa hiyo kwa kujidhulumu. Hata watu wao (hao manabii waliopita) waliwalaumu lakini yeye akaziondolea mbali (lawama hizo) na akasema kwamba yeyote anayewatolea kasoro yeye mwenyewe ndiye anakuwa ni mwenye kasoro.

MALIPO KWA MASIKINI

Ni masikini ndio huwa wa kwanza kujiunga na Jumuiya za Manabii. Ilmuradi Herakuli pia alimuuliza hivi hivi Abu Sufian kwamba A ashrafun naasit taba'uu am dhwu'afaa uhum. (Bukhari Kitabu badail Wahyi babu kaifa kaana bada ul Wahyi ilaa Rasuulil Laahi s.a.w.) lakini wakati Jumuiya inapoimarika na fedha zinaanza kuja basi ndugu na jamaa zao huanza kujifanya wenye kuzimiliki na kuanza kugawana wenyewe. Lakini yeye alisema kwamba vizazi vyangu hata wawe masikini au matajiri, hawatakuwa na haki yoyote katika mali hizo zinazokuja. (Bukhari Kitabuz Zakaat, babu maa yudhkaru fis sadaqati lin Nabiyyi (S.a.w.).
Masikini waliihudumia dini na hiyo haikuwa hisani yoyote ile kwa Mtume s.a.w. Bila shaka kidhahiri walikuwa wakimsaidia, lakini kwa hakika huo ulikuwa ni msaada wa nafsi zao wenyewe. Lakini hata hivyo yeye akauthamini msaada wao huo mdogo kwa kiasi hiki kwamba hadi akasema kwamba sisi tunawapa hata haki za watoto wetu hata kama ni masikini kiasi gani.

SIFA ZA MALIKI YAUMID DIIN

Sifa ya nne imeyobainishwa humo ni ya Maaliki yawmid diin. Yaani Mmiliki wa siku ya malipo. (Al Faatiha : 4). Na mmiliki huwa anakuwa ni yule ambaye huwa ni mwenye kukiwazia kitu chake tangu mwanzo. Mtumishi atasema tu; sawa itataangaliwa lakini mmiliki atayafikiria mambo yote tangu mwanzo kwamba isije ukatokea ugomvi. Na Mtume s.a.w. alithibitika kwa namna hii kuwa alikuwa ni mmiliki wa siku ya malipo kiroho kwamba makosa yote ambayo mwanadamu anaweza kuyatenda, yeye aliwaeleza njia za kuyazuia. Sisi twaona duniani kwamba jaji fulani anampa mwizi adhabu lakini hafanyi mpango wowote wa kuzikomesha sababu hizo zinazosababisha wizi.

Dini zimezobakia zimetoa fundisho hili kwamba mkorofi aadhibiwe lakini yeye s.a.w. aliufunga mlango wa ukorofi. Upande mmoja alijenga hali ya mtu kutosheka na kusema usiwe mwenye tamaa. Kisha kutokana na wazo hili kwamba masikini asilazimike kuiba kutokana na mahitajio, akaweka mfumo wa Zaka na sadaka. Badhi ya dini zimeagiza kwamba msizini lakini yeye akaamuru kwamba msitazame mtazamo mbaya.

Waambie waaminio wanaume wainamishe macho yao (24:31)
Na waambie wanawake waaminio wainamishe macho yao (24:32)
Iliyo chanzo hasa cha zinaa. Na kisha katika sura ya kutotosheka (kijinsia) ametoa ruhusa kwa mwanadamu kuoa hadi wanawake wanne kwa ajili ya kumuepusha mwanadamu na khulka mbaya.

Basi waoeni wanawake wawili au watatu au wanne muwapendao (4:4).
Kana kwamba hakutenda kama hakimu bali alitenda kama mmiliki. Hakuna mmiliki yeyote asemaye kwamba mtumishi akiwapiga wanyama wangu basi nitamuadhibu bali yeye humzuia tangu mwanzo kwa kumwambia usiwafanyie ukatili wanyama. Kwa kuwa yeye alikuwa ni mdhihirisho wa sifa ya Maalik, hivyo alikuwa ni mwenye kututakia wema zaidi kuliko sisi wenyewe. Kulikuwa na sahabi aliyekuwa akifunga saumu mchana kutwa na usiku alikuwa akikesha, basi akamkataza na kumwambia kuwa mkeo pia anayo haki kwako, jirani anayo haki na nafsi yako inayo haki kwako. [Maswnad Ahmad bin Hanbal jal. 2, uk 200 (Maswnad Abdullah bin Amr r.a. chapa ya Beirut ya mwaka 1978)], Yaani nafsi yako inayo haki kwako, kana kwamba mmiliki amwelezavyo mtumishi wake usimkimbize farasi wangu kwa kasi, Naye pia alisema hivyo hivyo.

MDHIHIRISHO KAMILI WA SIFA ZA MWENYEZI MUNGU

Madhumuni haya ni mapana kiasi hiki kwamba haiwezekani kwa wakati huu kuyaeleza ila tu kwa ishara, na sifa zote hizi nne zilikuwa zimepatikana ndani mwake kwa namna hii kwamba inafahamika kwa uwazi kabisa

Endelea uk. 5

Toka risasi kuchanua hadi ujengaji wa hoja

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Ukombozi wa nchi iwe kwa njia ya mazungumzo au kwa kutumia mtutu wa bunduki si lelemama asilani. Lakini ukombozi wa kweli na uliokamilika ni pale unapojitambua, unapoenzi na kutukuza kilicho chako. Kwa sudi ya ajabu Brigedia Generali Hashim Mbita alifanikiwa katika kushiriki katika ukombozi wa Afrika na katika kufanya Mtanzania ajivunie utanzania wake na kuona fahari ya kuwa mwana wa nchi hii. Mchango wa Brigedia Generali Hashim Mbita katika ukombozi wa Afrika ni kitabu kilicho wazi, ameshiriki kikamilifu na kuliletea taifa letu heshima kubwa. Hata hivyo sehemu ya pili ya mchango wake katika kukamilisha ukombozi wa Tanzania umejikita katika mapenzi yake makubwa ya kuendeleza, kulinda na kuheshimu lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Mapenzi yake juu ya Kiswahili yanatukumbusha wapenzi wengine mahiri wa Kiswahili akiwemo Shabaani Robert, Mwalimu Nyerere, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Mathias Mnyampala kuwataja wachache.

Brig - Gen Hashim Mbita

Tatizo letu kubwa kama taifa ni kutobaini kwa haraka vipaji vya watu wetu. Ni wachache wanaofahamu ya kwamba Mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa Mshairi wa jina. Ni wachache Zaidi wanaoweza kunasibisha Brigedia Generali Hashim Mbita na ushairi, lakini katika maisha yake Hashim Mbita alitunga mashairi ya kuisaidia jamii ijitambue.

Ni wachache pia wanaofahamu ya kuwa Brigedia Generali Hashim Mbita alikuwa Afisa wa Habari Mkoani Tabora wakati Mkuu wa Mkoa alikuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Wote wakipenda mashairi na alinieleza ya kwamba walikuwa wakipata fursa ya kuzungumza juu ya ushairi. Brigedia Generali Hashim Mbita alihamishiwa Mjini Dar es salaam kuwa Afisa Habari na hatimaye alichaguliwa kuwa Mwandishi wa Habari wa Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa mara ya pili wapenzi wa Mashairi walikutana. Safari hii Ikulu. Na ni dhahiri ya kwamba Hashim Mbita alifahamiana na washairi wote waliokuwa wanaishi mjini Dar es salaam akiwatembelea na kutayarisha mikutano yote ambayo Mwalimu J. K. Nyerere alikuwa akiwaita mara kwa mara kwenda Ikulu. Na mara nyingi Brigedia Generali Hashim Mbita alikuta anaulizwa na Mwalimu J. K. Nyerere vipi mbona hujawaita jamaa zangu washairi? Ni kwa njia hiyo masuala mengi yanayohusu Kiswahili kama uzinduzi wa vitabu, makongamano yanayohusu Kiswahili n.k hayo yote aliyashughulikia Brigedia Generali Hashim Mbita na kuhakikisha kwamba Mwalimu J. K. Nyerere hakuweza kukosa. Kwani alikuwa na mtu ambaye mara kwa mara alikuwa akimkumbusha juu ya mambo yanayoendelea katika ulimwengu wa Kiswahili. Tamasha lililofanyika ukumbi wa IFM wakati wa kuzindua utenzi mrefu kuliko zote katika lugha ya Kiswahili "Rasi-ul-Ghul" ulionesha bidii kubwa aliyokuwa nayo Brigedia Generali Hashim Mbita pamoja na Mwalimu J.K. Nyerere katika kukienzi Kiswahili. Ni katika tamasha hilo Mwalimu Nyerere alipoeleza jinsi Padri mmoja huko Bagamoyo alivyoweza kuupata utenzi huo kutoka kwa wenyeji wa Bagamoyo. Hii inatoa somo moja kubwa ya kwamba zipo kazi zetu nyingi sana ambazo watu wanazo lakini kwa bahati mbaya hazina wachapaji. Kuna hatari kubwa ya kwamba hazina zetu hizo zinaweza kupotea kama bidii ya makusudi haikuweza kufanywa.

Ni watu kama akina Brigedia Generali Hashim Mbita na Mwalimu J.K. Nyerere ambao walithamini sana mchango wa Kiswahili katika kuleta maendeleo ya nchi. Mara kwa mara washairi walikutana na Mwalimu J. K. Nyerere kuhusu Sanaa nzima ya ushairi, na aliweza kufuatilia hata migogoro iliyokuwa inaendelea katika ushairi wa Kiswahili. Ni katika mikutano ya namna hiyo ndipo Mwalimu J.K.Nyerere alipowahimiza washairi watunge mashairi siyo kwa kulazimishwa ila kwa kuelewa wanachokizungumza. Na akasifu utunzi wa ngonjera katika kuhamasisha wananchi ili wajiletee maendeleo. Katika hafla moja Mwalimu Nyerere alimuuliza Hashim Mbita; "Wako wapi vijana wanaotuimbia ngonjera?". Matayarisho hayakuwepo na Mwalimu akamueleza Bw. Hashim Mbita; "Kama tunakutana katika masuala yanayohusu Kiswahili ni vizuri tuanze na burudani ya mashairi".

Ni Hashim Mbita pia ambae aliuitisha mkutano wa Washairi hapo Ikulu na kuzungumzia na kuwaeleza Washairi nafasi ya ngonjera katika kuhamasisha umma wa Watanzania ili kujiletea maendeleo.

Mchango mwingine mkubwa wa Brigedia Generali Hashim Mbita katika kukienzi Kiswahili ni vile alivyoshughulikia muswada wa Mshairi maarufu Bw. Mathias Mnyampala ambaye aliandika juu ya maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi. Katika hali yake ya kuumwa umwa, mkutano uliweza kufanyika nyumbani kwake Chang'ombe akaweka mipango na mikakati kadhaa ya kufanikisha uzinduzi huo. Kazi ilifanyika usiku na mchana, washairi maarufu wakaingia katika kamati hiyo pamoja na wana Diplomasia na mipango yote ya uzinduzi ikawa imefanikiwa sana. Waliokuwa katika kamati hiyo ni pamoja na Bw. Amiri Sudi Andanenga, Bw. Suleiman Hega, Dr. Ahmad Kiwanuka, Bw. Jaafari Msolomi, Bw. Amir Abedi Kaluta na mwandishi wa Makala haya. Kila aliyemuona anashughulikia uzinduzi wa kitabu hicho cha Mathias Mnyampala alipata ushahidi wa kutosha kwamba Hashim Mbita alipenda sana maendeleo ya Kiswahili. Ikumbukwe ya kwamba uzinduzi wa kitabu hicho ulifanyika katika ukumbi wa Karimjee alipokuwepo pia balozi Job Lusinde na hotuba ya kusisimua ilitolewa na Mh. Kingunge Ngombale Mwilu.

Chama cha UKUTA kilipopata taarifa ya msiba wa Hashim Mbita kilifahamu kwamba kilikuwa kimempoteza mwanachama shupavu na hivyo likatolewa ombi chama cha UKUTA kipewe nafasi katika ratiba ya mazishi ya marehemu Hashim Mbita. Ombi hilo lilikubaliwa na Bw. Mohammed Saidi Manoro ambaye amewahi kuwa Katibu Mkuu wa UKUTA na sasa mlezi wa chama hicho alipewa fursa katika mazishi hayo kutoa neno la rambirambi. Yeye alisema ya kwamba; "Sisi washairi wa nchi hii tunamfahamu Hashim Mbita kama Jemedari aliyepambana katika vita vya kuleta heshima ya Watanzania kwa sababu hakuna vita kubwa kuliko ile ya kujenga utu wenu, utamaduni wenu na desturi zenu kwa ujumla". "Chama cha UKUTA kitaheshimu na kuenzi mchango wa Hashim Mbita" aliendelea kusema Bw. Manoro. Na kwa kumalizia aliweza kusoma shairi lililotungwa na Amir Sudi Andanenga la kumuaga Hashim Mbita.

Endelea uk. 6

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.

Kutoka uk. 4

kwamba yeye alikuwa ni mtu aliyekamilka kuliko wote, yaani alikuwa pia ni mwenye kuwakamilisha wengine. Hivyo kila mwanadamu mwenye kutazama uzuri na hisani anapaswa kumuheshimu.

DUA KWA ALLAH

Mwishoni ninamuomba Allah kwamba kwa kusudio lile tulilolianzishia siku hii, yaani kuzaa huba na upendo kati ya watu wa mataifa mbali mbali, litimie kikamilifu. Tabia na uwezo wa kuuona uzuri izalike miongoni mwa watu. Watu wote huutazama uzuri wa dhahiri lakini wenye kuuona uzuri wa asili ni wachache sana. Hakuna yeyote autazamaye ukweli wa hali ya juu na khulka njema, kwa kuwa watu hawana mazoea ya kuwaona manabii ambao Mwenyezi Mungu Amewaumba kama mdhihiriko wake. Mwenyezi Mungu Aiondoe hali hii ili watu waweze kuiona nuru Yake na upendo uzalike kwa wote, Wahindu, Masingasinga, Wakristo na Wazartasht. Waweze kuuona uzuri wa Manabii. Waweze kupata somo kutokana na mifano mema iliyomo ndani ya kila kaumu, Budha, Krishna na Zartasht, kwa uchache matukio ya aina hii yanapatikana katika maisha ya Manabii wote ambao kwao Waislamu wanaweza kujifunza. Mwenyezi Mungu Ameumba uzuri kila mahali nami naomba dua kwamba Awape watu uwezo wa kufaidika na uzuri huu. Mtume s.a.w. alikuwa ni wa kutiiwa na wote na aliyejumuisha ndani mwake uzuri wa wote, lakini mifano ya uzuri yapatikana ndani ya kila kaumu. Hivyo tazameni kila aina ya uzuri na muuangalie kila wema.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesemwa kuwa ni Mwanamfalme wa amani nami namuomba Allah dua kwamba Awape watu uwezo wa kulifahamu jambo hili kwamba njia ya amani ndio hii tu. Nasi pia Atujaalie uwezo wa kujenga amani na suluhu duniani na Atulinde na kila aina ya kuteleza Amin.

(Naashir Book Depot, Taalif wa Ishaat, Qadiyan, December 1933).

Bustani ya Washairi

NAMSHUKURU MANANI

1. Jina lake Mwenye Shani, utunzi ninaanzia
Kanijalia Kalini, kuitoa yangu nia
Nimevuka mitihani, mingi sana ya dunia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

2. Hapa nilipofikia, namshukuru Manani
Amenitoa gizani, kwenye nuru kuingia
Nilipata mitihan, nikalia na dunia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

3. Nilienda kisimani, huku nikiyawazia
Walisema mitaani, mengine nilisikia
Mimi nilijiamini, kweli nilivumilia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

4. Nilikuwa mashakani, niliwaza na kulia
Kuomba sikutamani, wala sikufikiria
Namshukuru Manani, nia kuniingizia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

5. Niliomba mkekani, sujda kuangukia
Nikaomba kwa makini, ndipo kanifunulia
Jamani sikuamini, kichwa nilishikilia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

6. Nilikuwa furahani, kuwa safi yangu njia
Nilikuwa masikini, niliomba kwa Jalia
Kwa kweli nimeamini, mkekani ndio njia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

7. Ndugu zangu wa Imani, jamani nawaambia
Mukipata mtihani, rudi kwa Mola Jalia
Musiseme kwa jirani, shetani takuingia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

8. Kimuomba kwa makini, chochote kitamania
Atokuacha njiani, Yeye takufikiria
Nawaambia jamani, njia bora kwenye dua
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

9. Kipato change shambani, wengine munalijua
Kukicha jembe begani, riziki jitafutia
Nitatunza bustani, hata nivune bamia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

10. Namuomba Rahmani, Anifungulie njia
Naimiliki bustani, kesho nifuge ngamia
Na dini nisiwe chini, japo nipate lupia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

11. Ninapokua juani, maombi kujisomea
Ninafunga Ramadhani, nne nguzo kutimia
Haniachi taabani, anajua yangu nia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

12. Japo hali yangu duni, sitomuacha Rabia
Hata kiwe kiganjani, mchango najitolea
Yeye ndiye muhisani, kesho tutapofikia
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

13. Kalamu naweka chini, hapa ninamalizia
Kweli ndugu wahisani, toba iwe ndio n jia
Utakuwa wa thamani, hilo ukiliwania
Namshukuru Manani, hapa nilipofikia

Bi. Rehema Fadhili –
Kitonga, Dar es salaam.

UTENZI

1 Twende kuwahubiria
Wasio Ahmadiyya
Ili kuwapelekea
Ujumbe wa Masihia

2 Siku zote wanangoja
Kuwa Yesu atashuka
Wakigoma na Unguja
Wote wanamngojea

3 Tena wanavyoamini
Atatokea mbinguni
Akishuka mawinguni
Kamwe haitatokea

4 Ni wamfano sikia
Siyo mwana wa Maria
Mtume ametwambia
Yesu alishajifia

5 Mwili wake kaburini
Roho yake imbinguni
Hatorudi asilani
Waache kumngojea

6 Wamfano amefika
Mtume alotukuka
Amekwisha dhihirika
Sisi tumempokea

7 Jina lake sikieni
Ni Ahmad jamani
Mzaliwa Kadiani
Na waje kumpokea

8 Waje kwake kwa haraka
Wajipatie baraka
Iwapo watatucheka
Sisi tumewajibika

9 Enyi jeshi la Mahadi
Twendeni kwenye jihadi
Twanguke kifudifudi
Kwa sala ya tahajudi

10 Silaha zetu ni nini
Ni aya za Qur'an
Siyo mabomu jamani
Watumiayo wahuni

OMARY M. SEBUGE
Mtibwa – Morogoro.

1 Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia
Swiraatwa kweli thabiti, isiyo na pingamizi
Kaiwezesha Rabana, Hamadia chombo kweli
Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia

2 Rabana tupe uwezo, tusukume gurudumu
Kwa kalamu na miomo, Hamadia idumishwe
Wale wanaoipinga, hukumu ni mbele yake
Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia

3 Kuanza kwa Hamadia, sisi tulikuwa bado
Hamadia ilianza, enzi za kale zamani
Rabana kawawezesha, waliotutangulia
Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia

4 Hamadia chanzo chake, Rabana kaiwezesha
Wote waliojiunga, wana maadili mema
Wafuasi wenye shani, wanavutia usoni
Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia

5 Kalamu naweka chini, hizo tano zinatosha
Kaniwezesha Rabana, ili nikupe ujumbe
Siwezi eleza mengi, ila machache pokea
Ukiutaka ukweli, ungana na Hamadia

J. Whalesi Rweikiza Kapima
Mwarazi Jamaat – Morogoro

KWA HERI HASHIMU MBITA (SHAIRI)

Kutoka uk. 5

1 Kwa jina la Rahamani, Rahimu mwenye nemsi
Wa mbingu na Ardhini, wa Ajinani na Insi
Twaomba yako hisani, umfanyie wepesi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita.

2 Mpendwa Hashimu Mbita, mwingize Firdausi
Mazuri endekupata, ndivyo tuombavyo sisi
Vikwazo vyote kupita, bila zingo na tatasi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita

3 Alikuwa muhimili, kiranja kwenye kikosi
Katika taifa hili, kuwafukuza waasi
Na lugha ya Kiswahili, katetea umilisi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita

4 Na katika ukombozi, hakuwa na wasiwasi
Katika kuzamambizi, kutafuta ufanisi
Hadi kwenye ufumbuzi, kwa hali na kwa risasi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita

5 Hashimu katika lugha, kujibu na kudadisi
Mantiki na balagha, alikuwa ni Rafisi
Ndimi za kuyughayugha, hazikuwa na nafasi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita

6 Twakuomba Ya-Rahimu, Ya-Ilahi ya Kudusi
Ilivyo Mwanaadamu, kufariki sio basi
Kuna maisha matamu, twaomba ende jalisi
Mwingize Firdausi, mpendwa Hashimu Mbita

Amiri Sudi Andanenga - Sauti ya kiza (Bahari-El-Ulumu)

Usomaji wa shairi hili katika mazishi hayo ndiyo kitu kilichoonesha sehemu muhimu ya utamaduni wetu. Baadhi ya mabalozi wa nchi zilizowakilishwa katika mazishi hayo waliomba nakala ya shairi hilo. Kwa mara nyingine hata wakati hayupo Hashim Mbita akaendelea kung'arisha utamaduni wa nchi yetu. Ingawaje mwandishi yule maarufu wa Uingereza Shakespear katika mchezo '*Julius Kaisari*' uliotafsiriwa kwa Kiswahili na Mwalimu J.K.Nyerere anasema; "Maovu wayatendayo binadamu huishi wakishakufa, mema huzikwa nayo" lakini hiyo haikuwa hivyo kwa shujaa wetu. Mema aliyoyatenda shujaa wetu tunaendelea kuishi nayo kama vile kuenzi ushairi wa Kiswahili kama lilivyosomwa katika mazishi hayo.

1 Kiswahili ni yatima, kumpoteza mzazi
Kakilea kwa adhama, mapenzi yaloazizi
Sisi tulobaki nyuma, turutubishe mizizi
Ili nasi tuwakoge, walotukoga zamani.

2 Sisi tulobaki nyuma, turutubishe mizizi
Lugha tuipe heshima, tuache yetu ajizi
Lugha ni wetu uzima, lugha ni letu jahazi
Utavukaje bahari, wakati huna jahazi?

3 Lugha ni wetu uzima, lugha ni yetu jahazi
Kwa lugha tunasimama, na kusafiri shamazi
Bila lugha ni nakama, chochote hatukiwezi
Mko wapi watetezi, wa lugha yetu ya mama?

4 Wa lugha yetu ya mama, mko wapi watetezi?
Tafadhali njoo hima, haraka tujenge zizi
Tuilinde na wanyama, wenye inda walowezi
Kisitawi Kiswahili, roho ya taifa letu

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

Sir Muhammad Zafrullah Khan - sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa aliyetembelea Tanzania akiwa Mgeni wa Serikali

Na Mahmood Hamsin Mubiru – Dar es salaam

Historia iliyotukuka ya taifa la Kiislam la Pakistan lililoasisiwa mwaka 1947 na Qaid-ul-Azam Muhammad Ali Jinnah inaonesha mchango adhimu wa taifa hilo katika kutetea haki za wanyonge bilkhusi ukombozi wa nchi zilizokuwa chini ya ukoloni na dhuluma kubwa waliyotendewa Wapelestina kwa kunyang'anywa ardhi yao kwa kupitia vitimbwi, hila, ulaghai desturi kubwa ya Waingereza.

Muhimili wa sera za nchi za nje wa taifa la Pakistan aliyesaidia katika kueleza na kuimarisha mtizamo wa nchi hiyo kuhusu mambo ya nchi za nje hakuwa mwingine isipokuwa sahaba maarufu wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as), mwanasheria maarufu, mwanadiplomasia, mwandishi wa vitabu na mwanasiasa mwenye jina Sir Muhammad Zafrullah Khan.

Hotuba zake katika Umoja wa Mataifa zilipinga ukoloni, ubeberu na maonevu. Kazi yake hii nzuri ilienea sehemu nyingi duniani na Waarabu kutokana na mchango wa kutetea haki za Wapalestina alipewa lakabu ya 'Simba wa ukombozi' na nchi ya Saudia Arabia ilimfanya kuwa mgeni wa heshima wakati alipokwenda kufanya Hija katika nchi hiyo.

Mungu bariki katika miaka ya 1940 tulikuwa na Masheikh waliokuwa wanajuna fika na mtetezi huyo wa wanyonge. Walijuana kwa sababu wote walikuwa ni Wapakistan, lakini la msingi zaidi ni kwamba wote walikuwa ni Wanajamaat. Sheikh Mubarak Ahmad Mbashiri wa kwanza wa Ahmadiyya katika Afrika ya Mashariki alifahamiana vilivyo na waziri huyo wa mambo ya nchi za nje wa Pakistan. Sheikh Abdulkarim Sharma ambaye aliwahi kuwa Amir nchini Uganda na kuwa Amir nchini Tanzania naye pia alikuwa akifahamiana vilivyo na Sir Muhammad Zafrullah Khan. Hivyo vuguvugu la siasa lilipokuwa linaendelea nchini wazo lilitolewa ya kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kiongozi wa TANU afunge safari ya kwenda katika Umoja wa mataifa ili kuwakilisha kilio cha Watanganyika katika mji wa New York. Ikumbukwe ya kwamba Tanganyika ilikuwa chini ya udhamini wa Umoja wa mataifa na hivyo ndio wao waliokuwa wamepewa udhamini wa kusimamia nchi hii. Mjadala mrefu uliendelea baina ya Sheikh Mubarak Ahmad, Sheikh Abdulkarim Sharma na Mwalimu Nyerere wakizungumzia mambo ambayo alitakiwa ayawakilishe kwenye baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa. Mazungumzo hayo yaliweza kuibua mawazo yaliyokubaliana kuhusu yale ambayo angeweza kuyawakilisha katika umoja wa mataifa. Lakini la muhimu zaidi ni kwamba alipewa barua maalum ya utambulisho na Sheikh Mubarak Ahmad ili aipeleke kwa Sir Muhammad Zafrullah Khan ambaye alikuwa anawakilisha Pakistan katika Umoja wa Mataifa. Na kwa sababu Sir Muhammad Zafrullah Khan alikuwa ni mwanasheria aliyebobea walimuomba ampe ushauri unaofaa katika kutekeleza azma hiyo ya kutetea watu wa Tanganyika.

Sir Muhmmad Zafrullah Khan (anayepunga mkono) alipowasili uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Dar es Salaam wakati alipoitembelea Tanganyika akiwa mgeni wa Serikali.

Ni muhimu kuweka jambo moja wazi, sawa na hali ya kisiasa iliyokuwa katika miaka ya 1940 na 1950, Mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa karibu sana na Waislam na alishirikiana nao katika mambo mengi. Habari za Mwalimu kufunga saumu, na kwenda Bagamoyo amezieleza vizuri yeye mwenyewe. Ni dhahiri kuwa Mwalimu Nyerere alilazimika kuwa karibu na Waislam kwa sababu Kanisa Katoliki lilikuwa haliungi mkono hata kidogo mapambano ya uhuru. Kwa ujumla Ukristo ulikwenda kinyume na dhamira ya Watanganyika kujitawala. Huko sehemu za Mwanza na Bukoba 'Church Mission Society' (CMS) lilipiga marufuku waumini wake kujiunga na chama cha TANU. Kama tulivyokwisha bainisha ni Waislam ndio waliomsikiliza Mwalimu Nyerere na kufanya nae kazi bega kwa bega. Mwanahistoria Mohammed Saidi ametizama kwa undani mchango wa Waislam katika harakati za kuleta uhuru na ameonesha ukarimu mkubwa walioufanya Waislam katika kumpokea na kumkubali na kumsaidia Mwalimu Julius K. Nyerere.

Mchango wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya katika siku za mwanzo za kuanzishwa kwa chama cha TANU ni mkubwa sana. Barua za chama zilikuwa zikichapwa hapa Makao Makuu na Nyerere alikuwa akitembelea Makao Makuu mara kwa mara. Ndiyo maana upo ushahidi ya kwamba safari yake ya umoja wa Mataifa waliijadili Mwalimu Nyerere pamoja na Sheikh Mubarak Ahmad na Sheikh Sharma ambao waliweza kumpa mawaidha mazuri na kama tulivyokwisha sema walimpa barua ya utambulisho kwa Sir Muhammad Zafrullah Khan.

Mwalimu Nyerere alikutana na Sir Muhammad Zafrullah Khan katika jiji la New York. Walikuwa na mazungumzo marefu na akampa mashauri yaliyohusiana na sheria pamoja na siasa. Hotuba ya Mwalimu Nyerere ilikuwa gumzo jijini New York na nje ya jiji hilo. Kwa hali ya utulivu na kujiamini Mwalimu alieleza maumivu ya watu wa Tanganyika bila kuonesha aina yoyote ya chuki na alionesha kabisa ya kwamba alilokuwa analisema amelifanyia utafiti na ana ushahidi nalo. Hotuba hiyo ilipokelewa kwa shangwe kubwa na vigelegele na kutokana na uzito na uzuri wa hotuba hiyo ilishauriwa na chama cha TANU ya kwamba itafsiriwe katika lugha ya Kiswahili. Nae Mwalimu Julius K. Nyerere hakuwa na tatizo la kumpata mtu wa kutafsiri hotuba yake hiyo kutoka kwenye lugha ya Kiingereza kwenda kwenye lugha ya Kiswahili kwani alimfahamu Sheikh Kaluta Amri Abedi kwamba alikuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo. Kazi hiyo ilifanyika na mwisho wake kikatolewa kitabu kiitwacho '*Kilio cha Uhuru*'.

Moja ya sifa ya Mwalimu katu hakusahau ikhsani aliyofanyiwa huko nyuma. Tumekwishaona alivyotetea uwanja wetu wa Morogoro uliotakiwa kuchukuliwa. Tumekwisha kumuona pia akihudhuria tafrija ya kumuaga Sheikh Mubaraka Ahmad aliyekuwa anakwenda likizo Pakistan. Tumekwisha pia kumuona alivyowakaribisha Masheikh wa ki Ahmadiyya katika tafrija ya kusherehekea uhuru katika viwanja vya Ikulu jijini Dar es Salaam. Hizo zote ni dalili za kuonesha ya kwamba alikuwa na uhusiano wa karibu sana na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Wengi wanapopata vyeo husahau yote ya nyuma, lakini Mwalimu Nyerere hakuwa hivyo.

Hata baada ya kuwa Waziri Mkuu mwaka 1961 na Rais wa Jamhuri ya Tanganyika mwaka 1962 hakuweza kuwasahau wale waliomsaidia wakati wasaidizi hawakuwepo. Rais wa baraza la Umoja wa Mataifa kwa wakati huo Sir Muhammad Zafrullah Khan aliyepata pia kuwa Jaji wa Mahakama kuu ya dunia (The Heague) alipewa mwaliko rasmi na rais wa Jamhuri ya Tanganyika Mwalimu Julius K. Nyerere kuitembelea nchi. Ilikuwa ni alama ya kukumbuka mchango wa Wakili wake wakati akiwa Umoja wa Mataifa.

Safari ya Sir Muhammad Zafrullah Khan ilikuwa ni ya kiserikali tangu mwanzo hadi mwisho. Hata hivyo wale waliojaaliwa kutanguliza dini mbele ya dunia kama alivyokuwa Sir Muhammad Zafrullah Khan, yeye alihakikisha kuwa Jumuiyya ya Ahmadiyya inashiriki kikamilifu katika ziara yake. Katika uwanja wa ndege wa kimataifa Rais alimtuma makamu wake wa Rais Mh. Rashidi Mfaume Kawawa pamoja na Waziri wa viwanda wa wakati huo Akhsante Rabbi Nsilo Swai ambao walikwenda kumpokea, pamoja nao alikuwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry na binti mmoja wa Kiahmadiyya alimvisha mgeni shada la maua.

Kutoka uwanja wa ndege aliwaomba wanaoongoza msafara wapite kwanza Masjid Salaam. Wanajumuiyya walimlaki hapo msikitini na baada ya mapokezi hayo akaelekea Ikulu ambako alikuwa na mazungumzo na mwenyeji wake Mwalimu J. K. Nyerere.

Usiku huo Jumuiyya ya Ahmadiyya ilikuwa imetayarisha dhifa katika hoteli ya New Africa. Ambako takribani mawaziri wote walihudhuria isipokuwa Mwalimu Nyerere aliyekuwa na udhuru. Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini wote walikuwa wamepewa mwaliko na waliweza kuhudhuria. Hotuba ya Sir Muhammad Zafrullah Khan ilikuwa maana ya Islam kwa mtu wa leo. Watu walitoa sifa mbalimbali kwenye dhifa hiyo. Kwanza ufafanuzi wa kuvutia kuhusu Islam ambapo Sir Muhammad Zafrullah Khan

Endelea uk. 8

Tukumbuke kule tulikotoka

Na Mwandishi wetu
Dar es Salaam

Katika zamani zile Jiji la Dar es salaam lilikuwa na Masheikh kadhaa maarufu, lakini waliosikika sana ni hawa wafuatao: Msomi Abdullah Idi Chaurembo, Sheikh Abdullah Khan, Sheikh Ashir, Sheikh Hassan Bin Amiri, Sheikh Idirisa, Mzee Komorian, Sheikh Mohammed Ally Ngongabule na Sheikh Suleiman Takadir. Sheikh Ngongabule, Ashir na Abdullah Khan walikuwa Mashiya na waliobaki walikuwa Suni. Lakini wote kwa pamoja walishirikiana kuipinga Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Wakiwa Misikitini mwao, Masheikh hao walikuwa wanawakataza wafuasi wao wasizungumze na wa Ahmadiyya kwa masuala ya dini kwa sababu wana hoja nzito nzito nao hawana wajuwalo, kwa hiyo ni rahisi kukubaliana nao. Masheikh hao wengi wao walikuwa woga wa mazungumzo hasa kadamnasi. Hawakujitokeza dhahiri kujadiliana na Ahmadiyya, bali huyu Sheikh Abdullah Khan ambaye alikuwa Mshia ndiye aliyejitokeza. Alikuwa anazunguka huku na huko mitaani kujaribu kuwaeleza watu ukafiri wa Jumuiyya ya Ahmadiyya. Aliifanya kazi hiyo kwa juhudi yake yote. Kwa kuwa yeye ni Mhindi, alikuwa anadai kwamba anamfahamu vizuri mwanzilishi wa Jamaat Ahmadiyya, lakini alipokutana na Wabashiri wa Jamaat Ahmadiyya alikaushwa mate.

Pamwe na kukaushwa mate, alibaki na maneno ya kebehi na matusi tu mdomoni mwake. Hoja zake zote zilipata majibu ya kielimu. Wale watu ambao pale mwanzo walikuwa upande wake wakampuuza na kumfanya hamnazo. Mwanafunzi wake mmoja ambaye alikuwa naye katika kazi ya kupinga Ahmadiyya, alikuwa anafuatilia kwa makini sana juu ya maelezo yaliyokuwa yanatolewa na Ahmadiyya. Yalikuwa yanamwingia vyema. Kilichotokea ni kwamba mwanafunzi huyo alijiunga katika Jamaat Ahmadiyya, si mwingine bali ni Mwalimu Daudi Ally Shoo.

Mzee Rashidi Msabaha ambaye naye alikuwa mwanafunzi wa Sheikh Hassan Bin Amir akajiunga na Jamaat Ahmadiyya pia.

Ni wakati wa vuguvugu kubwa la kudai uhuru. Vyama kadhaa vya siasa vilianzishwa ukiacha TANU ambayo ilitangulia, pia palikuwapo African National Congres, Amnut na UTP. Vyote vilikuwa vya kisiasa katika mbio ya kutafuta uhuru. Kilichojiri ni kuwa baadhi ya hawa Masheikh wakajiingiza

Wakati wa mazishi ya Sheikh Kaluta Amri Abedi masheikh mbalimbali wasio Waahmadiyya walishiriki

kwenye vyama hivi kichwa kichwa. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati huo ndiye alikuwa kiongozi wa TANU. Akiwa na wadhifa huo alifika Masjid Salaam karibu mara tatu hivi. Alifika Msikitini hapo kumfuata Sheikh Kaluta Amri Abedi. Inaonesha Mwalimu alifikiri hekima na busara ya Sheikh kwa hakika alimuweka miongoni mwa washauri wake mashuhuri.

Nakumbuka tena vizuri sana kwenye mkutano mmoja wa hadhara pale Jangwani alishangaza watu na kuwaacha vinywa wazi. Japo mimi siwezi kuandika neno kwa neno aliyotamka siku ile, lakini alinena; "Mimi ni Mkristo halisi, kama hivi sasa nitaamuwa kujiunga katika Islam, kwa kweli nitajiunga katika Ahmadiyya". Akakazia tena; "Sababu ninayo" (huenda alitamka hayo kwa utani), lakini ukweli utabaki kuwa ukweli.

Alhamdulillahi uhuru tukaupata tukajitawala wenyewe. Ndio wakati ambao Masheikh wa Dar es salaam walipoongeza uhasama kwa Jumuiyya ya Ahmadiyya. Kwa wakati ule Dar es salaam ilikuwa na wanachama wachache wa Jumuiyya , lakini walionekana wengi machoni mwa wapinzani. Wanajumuiyya hao wachache walitakiwa kumwomba sana Mwenyezi Mungu hali ile ya upinzani mkali ipowe na watu wapewe usikivu, Allah Aondowe gumbizi la wapinzani waweze kuuona ukweli wa Ahmadiyya. Kwa hiyo Wanajumuiyya walikubaliana kuamka usiku kila mmoja nyumbani kwake kwa ajili ya swala ya Tahajjud na kufunga swaumu za nafali.

Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi alipoteuliwa kuwa Waziri, alipewa nyumba ya kuishi kule karibu na Ikulu. Lakini baada ya swala zake za usiku, swala ya Alfajiri alikuwa anaungana na Wanajumuiyya wengine katika Masjid Salaam. Tuko kwenye Serikali ya wananchi, asubuhi moja tukasoma kwenye magazeti kwamba Sheikh Hassan bin Amir ameamriwa na serikali kuondoka Dar es salaam mara moja. Hatua hiyo ya Serikali ilikuja baada ya kubaini Sheikih hakutumia vyema nafasi yake, bali alileta kitu uchochezi kati ya Serikali na Waislam. Baadae ikafahamika kuwa Sheikh huyo aliibukia Zanzibar. Baada ya siku chache, tukaona kwenye gazeti Jeneza la Kisiasa la Sheikh Suleiman Takadir. Lilikuwa laonesha kumalizika kwa uhai wa siasa. Mazishi hayo yalitamkwa na Raisi wa TANU kwa wakati huo. Kwa nini? Kwa sababu Sheikh Takadir ni mpenda udini kitu ambacho kinaweza kuharibu siasa ya nchi yetu na kuhatarisha usalama. Masheikh wengine hata bila ya Serikali kuwachukulia hatua walikufa kihoro. Hayo yote yamesadifu beti za Sheikh Kaluta:

Wangapi wafile,
waliojipinda nayo zahama.
Walokwenda kule,
huku na huko wakituzoma.
Toka siku zile,
mpaka leo ninaposema.
Twapanda vilele,
tukikiuka vyote vilima.
Ole wenu ole,
imekuwaje kutotazama.

Ziwacheni kedi,
hii ni njia yake Karima.
Kaja Mauhudi,
Mahadi wenu mwenye adhama
Na Njema idadi,
ya wacha Mungu watu kirama
Wameona budi,
Mjumbe huyu kumuandama
Hujajua hadi,
takufaani hiyo tuhuma?
(Diwani ya Amri).

Sir Muhammad Zafrullah Khan

Kutoka uk. 7

alisema ya kwamba; "Islam inaamini ya kwamba maisha ni harakati, na hakuna sudusi ya muda wa kupumzika. Na katika harakati hizo hutokea hitilafu na migongano. Hata hivyo kutofautiana na ile hali ya kutofautiana ndiyo hasa chimbuko la elimu, utafiti na maendeleo. Wakati tunalinda haki ya kutofautiana kuuliza, kukataa, na wakati mwingine kupingana, lakini lazima tukumbuke kwamba tofauti zetu hizo zinazotokana na dini, falsafa, siasa zituletee faida na sio hasara. Na njia pekee ya kufikia lengo hilo ni kuwa tayari kusikiliza hoja inayojengwa na mwingine. Waliohudhuria dhifa hiyo walifurahishwa sana juu ya maelezo yake juu ya Islam. Na wengine walivutwa na uwezo wake mkubwa wa lugha ya Kiingereza. Inasemekana baadhi ya mawaziri walikwenda kumwambia Mwalimu Julius K. Nyerere "Umekosa dhifa ya kisomi". "Na mzee huyu akizungumza hapa mara mbili mara tatu hutompata Mkristo hata mmoja hapa nchini"; Mwalimu Nyerere alitabasamu na kusema; "Hao ndio Waahmadiyya, mimi nilikutana nao zamani huko Tabora".

Siku iliyofuata ilikuwa Ijumaa na Sir Muhammad Zafrullah Khan alipewa fursa ya kuongoza sala ya Ijumaa. Nilipata bahati ya kupata maelezo ya mtu aliyekuwepo katika sala hiyo, Bw. Alli Saidi Ndendekele. Yeye alinieleza Sir Muhammad Zafrullah Khan alitoa hotuba ya kusisimua na kuongeza imani. Yaliyotokea baadae yalikuwa ni funzo kubwa kwa Wanajamaat. Rais wa baraza la umoja wa mataifa aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya nchi za nje, aliyekuwa amevaa kofia ya tunga ambayo ilikuwa ya kawaida sana na usingefahamu rangi ya suruali yake aliyokuwa ameivaa kuwa ilikuwa na rangi gani hapo mwanzoni. Alikuwa ni mtu wa kawaida asiye na majivuno na mbwembwe. Wakati anaenda kuvaa viatu vyake Sheikh Muhammad Munawwar alitoka kwa kasi kidogo ili kumwekea viatu vyake sawasawa. Sir Muhammad Zafrullah Khan alikataa kabisa lakini maulana Sheikh Muhammad Munawwar alimwambia ninafanya hivi kwa sababu wewe ni sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na si vinginevyo. Hapo Sir Muhammad Zafrullah Khan hakuwa na la kusema na akakubali yale Maulana Muhammad Munawwar aliyokuwa anataka kufanya.

Upo ushahidi pia unaonesha ya kwamba Mwalimu Nyerere na Sir Zafrullah Khan waliendelea kuandikiana barua na kutumiana salamu. Sheikh Mubarak Ahmad alipotembelea Tanzania katika kutayarisha safari ya Mtukufu Khalifa wa Nne nchini Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) alipewa zawadi na Sir Zafrullah Khan ili amfikishie Mwalimu Nyerere. Zawadi hiyo ilikuwa ni kitabu cha Sir Muhammad Zafrullah Khan kinachoitwa '***My Mother***'. Wakati Sheikh Mubarak Ahmad anakuja nchini Mwalimu Nyerere hakuwepo nchini lakini zawadi hiyo ilipokelewa na mama Maria na baadae Mwalimu Nyerere alimuandikia barua Sheikh Mubarak Ahmad akimshukuru kwa zawadi hiyo.

Masimulizi yote haya yanaonesha ukaribu uliokuwepo baina ya Mwalimu Julius K. Nyerere na Waahmadiyya. Na iwapo mtu anahitaji kuelewa zaidi juu ya Mwalimu Nyerere, ushauri ni kwamba atafute uhusiano Mwalimu Nyerere aliokuwa nao na Waahmadiyya.

Kiswahili na ukombozi wa Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru – Dar es salaam.

Kiswahili kina sifa,
kwa nahau na maana.
Hufanya na mataifa,
mengi kusikilizana.
Kikitoa tarifa,
kwa wengi huwa bayana.
Na iwapo kitakufa,
roho nyingi zitatnuna.
Titi la mama ni tamu,
jingine halishi hamu.
(*Shaaban Robert*).

Nchi ya Tanzania imejichumia sifa nyingi zikiwemo za kuwa ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki kupata uhuru. Kuupata uhuru kwa njia ya Amani, na nchi kuendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu, na kama wasemavyo Waswahili; "*Ukiona vyaelea hapana shaka vimeundwa*". Na mchango wa Kiswahili katika muundo huo ni mkubwa na muhimu sana. Na hilo unaweza kulielewa tu ukikutana na jamii ambazo hazina bahati ya kuwa na lugha inayowaunganisha. Wanakuwa katika mahangaiko kiasi hiki ya kwamba wanalazimika kutumia lugha ya yule aliyekuwa anawatawala. Ni maumivu makubwa na fedheha. Tanzania tumetoka katika dimbwi hilo la aibu kwa kuwa na sudi ya kuwa na lugha moja inayotuunganisha sote na kuwa taifa. Na lugha hiyo ni Kiswahili.

Lugha ina nafasi muhimu katika kuwapa watu taadhima, mshikamano, kuendeleza na kuhifadhi mila na desturi zao. Na hivi ni vitu muhimu vinavyolipa taifa utambulisho na heshima. Kiswahili kinayo bahati kubwa ya kuwa lugha isiyonasibishwa na kabila au kundi fulani katika jamii. Ni dhahiri basi inaonesha Kiswahili ni mali ya wote. Jambo hilo la Kihistoria lilifanya Kiswahili kikubalike na kiwe kiunganishi kikubwa cha kuwaleta watu pamoja. Unapowaleta watu pamoja, wanakuwa na nguvu na maendeleo. Hapana shaka umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Tulihitaji sana umoja na maelewano wakati wa kupambana na wakoloni. Kiswahili kilikuwa na kinaendelea kuwa jiwe kuu la pembeni la maendeleo yetu na umoja wetu.

Akizungumzia juu ya mchango wa Kiswahili katika kutuunganisha, mshairi maarufu wa Kiswahili Sheikh Kaluta Amri Abedi anasema;
"Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu aliyejaalia Kiswahili kisemwe Bara na Pwani kwacho akawaunganisha wakazi wa jadi na walowezi walohitilafiana, makabila, na rangi na dini. Akawawezesha viongozi kutumia Kiswahili kiwafungue watu akili wakapambazukiwa na alfajri ya utambuzi iliyofuatana na asubuhi inawirishayo kwa wingi wa miale na mwangaza kamili. Kwacho wanyonge wakapata nguvu na ukakamavu wa kupambana na serikali yenye mabavu".

Baadhi ya washairi maarufu nchini akiwemo Sheikh Amri Abedi, Matias Mnyampala, Hemed Feruz Mbiyana, Dr. Lyndon Harris na wengineo

Inawezekana kabisa kuwa na mawazo mazuri, fikra safi na kwa hakika una mshawasha wa kuinusuru jamii yako. Mapenzi hayo yote yanaweza kutafsiriwa kwa vitendo iwapo una chombo cha kufikisha mawazo na fikra zako. Ni lazima unaowaeleza wakuelewe na wakubali hoja zako. Itakumbukwa ya kwamba, ujenzi wa mnara wa Babeli ulileta mushkili kwa sababu ya kutokuwa na chombo hiki muhimu yaani lugha ya kuwaunganisha wajenzi.

TANU ilikuwa na ujumbe mzito, ujumbe wa ukombozi. Ujumbe wa heshima na utu wa Mwafrika na ujumbe wa kujitambua. Ujumbe kwamba hakuna kiumbe bora wa kumtawala mwingine. Ujumbe ya kwamba tumenyanyaswa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, sasa tunataka kuwa mabwana katika ardhi yetu. Habari njema hii ingewafikia vipi wazalendo wa Tanzania bila lugha ambayo imeweza kuyaunganisha makabila 120 ya Tanganyika yaweze kuelewana? Mambo yangekuwaje bila lugha hiyo? Julius Kambarage Nyerere angefahamika vipi kwamba alikuwa na ujumbe mzito na pia alikuwa na uwezo wa kufafanua na kufikisha ujumbe huo? Ni Kiswahili kilichovusha jahazi letu lililokuwa linasafiri kutoka ardhi inayoitwa kutawaliwa hadi ardhi ya matumaini yaani ardhi ya uhuru.

Kazi hata hivyo haikuwa rahisi, kuhututubia mikutano ya hadhara, mashairi, vitabu hivyo vyote viliwasha moto wa uhuru na moto huo ukasambaa kama majani makavu yanayowaka wakati wa kiangazi. Serikali ya kikoloni ilitumia mbinu za kuhakikisha watu hawapati habari za ukombozi wao. Hata hivyo jitihada zilifanywa za kufikisha ujumbe huo kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa mathalani mwaka 1953, mwaka mmoja kabla ya kuzaliwa chama kilichopigania uhuru – TANU Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya iliyosajiliwa mwaka 1934 ilitafsiri Qur'an Tukufu katika Kiswahili, na kazi hiyo ilifanywa na Sheikh Mubaraka Ahmad. Mwito uliyomo humo ni mwito wa uhuru wa kweli, ni mwito kwa Waafrika kukata minyororo yao. Kumbuka hiyo ilikuwa ni mwaka 1953 na ukoloni ndio unanuka hasa! Lakini katika tafsiri hiyo kuna maneno ya kimapinduzi ya Kiongozi wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) ambaye anasema;
"**Nyinyi hamheshimiwi hata kidogo, hamko huru, mmo kwenye minyororo, na kitu cha kuwatoa kwenye minyororo hiyo ni kufuata mafundisho ya Kurani Tukufu yaliyowapa Waarabu wa Jangwani Elimu, Ustaarabu, ukombozi na maendeleo**".
Mashairi nayo yalitoa changamoto kubwa katika kuhamasisha umma ili ujikomboe. Kwa mfano Sheikh Kaluta Amri Abedi katika miaka hiyo ya hamsini anazungumzia juu ya uhuru.

Uhuru ni mawahibu, katoa Mola Mkwasi
Pamwe na kuukutubu, uenee kwa unasi
Uhuru jambo wajibu, kwa ajinani na insi
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Magazeti nayo yalifanya kazi nzuri ya kuhamasisha umma wa Watanzania. Magazeti yafuatayo yaliweza kutoa habari zinazohusu uhuru. Magazeti hayo ni pamoja na '*Msimulizi, Habari za Mwezi, Pwani na Bara, Rafiki yangu, Habari za Leo, Kwetu, Mamboleo, Muwangaza*, lakini gazeti lililofanya kazi kubwa na TANU ilikuwa na uhuru wa kulitumia lilikuwa ni gazeti la *Mapenzi ya Mungu* lililoanzishwa mwaka 1936 na kujipatia sifa ya kuwa gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa katika lugha ya Kiswahili. Hivyo likafanikiwa kutoa elimu kwa jamii na kuweza kukikuza Kiswahili.

Wanahistoria wengi wanaamini ya kwamba nchi za Afrika Mashariki Kenya, Uganda na Tanzania. Tanzania ilijitokeza ya kwanza kupata uhuru kwa sababu haikuwa na makabila makubwa yenye uhasama kama ilivyo Uganda na Kenya. Wanaeleza pia ya kwamba katika nchi za Kenya na Uganda palikuwepo na vyama vikubwa vyenye nguvu wakati Tanganyika palikuwa na chama kimoja chenye nguvu. Hizo wanajenga hoja ya kwamba ndizo sababu kubwa zilizofanya nchi za Kenya na Uganda zichelewe kupata uhuru wake. Ni kweli nchi ya Tanganyika haikuwa na makabila yenye uhasama kama ilivyokuwa nchini Kenya na Uganda. Hata hivyo sababu kubwa ya kupatikana kwa uhuru kwa haraka kwa nchi ya Tanganyika inasadikiwa ya kwamba ni kwa sababu ya lugha ya Kiswahili.

TANGAZO LA IJITIMAA YA LAJNA NA NASIRAT 2015

Tanzim ya Lajna Imaillah Tanzania inapenda kuwataarifu Lajna wote nchini kuwa Ijtimaa ya Lajna Imaillah itakuwa tarehe 12 – 14 Juni, 2015 Mkuyuni Mkoani Morogoro. In-Shaa-Allah.

Lajna na Nasrat wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Limetolewa na Katibu wa Ish'at wa Lajna Imaillah

Maungano na Mwenyezi Mungu ndio Msingi wa maendeleo yote

Kutoka uk. 11

maombi/sala na kumwabudu Mungu, pili kuzuia jazba zetu na kutafakari juu ya saikolojia ya mwanadamu na tatu mtu kuwa mkweli juu ya utaalamu wake na kujitahidi kujitafutia elimu zote ikiwemo elimu ya sayansi.

Iwapo tutafakari tutagundua kwamba ili kutimiza haki zetu wenyewe, sala na mafungamano na Mungu yanatufanya tuwe na uwezo wa kuzilinda hisia zetu. Uaminifu kazini unatongoza kwenye kukuza tabia njema, maendeleo ya kiroho na ya kidunia pia. Pia ili kutimiza haki za familia tunafanya maombi, tunazidhibiti hisia zetu na tunawatimizia mahitaji yao. Haki za majirani nazo zitaweza kutimizwa kupitia maombi, kuwajali mahitaji yao na kujaribu kuzielewa hali zao za ndani (mind-setup) ili kwamba ujumbe wa Islam uweze kufikishwa kwao ipasavyo. Kwa kufanya kazi kwa bidii tunakuwa wenye manufaa kwa jamii na iwapo kila mmoja atatekeleza hayo katika jamii basi jamii nzima itakuwa ni mfano bora wa tabia njema, maendeleo ya kiroho na maendeleo ya kidunia pia.

Hali ya kuhuzunisha mno kwa Waislam hivi sasa ni kwamba wametoa kipaumbele kwa mawazo yao binafsi na wakaweka kando mafundisho ya dini. Matokeo yake ni kwamba wanafikiria kuwa hayo wanayoyafanya ni matendo ya Kiislam, kumbe ni fikra tu zinazotokana na mawazo yao na hatimaye ni kuuana wao kwao. Kinachosikitisha zaidi wamepoteza kote; wamepoteza dunia, na wamepoteza kiroho. Na hivi sasa wao ni waombaji tu wanaopita wakiombaomba.

Nchi za Magharibi kwa upande mwingine zimetoa kipaumbele kwa mambo ya dunia na wakayapa kisogo mambo ya Imani, lakini angalau wao wamefaulu kupata shabaha za kidunia, ingawaje kwa kutumia njia potofu. Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa ili kuwatengeneza watu wa aina mbili hizi. Watu wanapofika katika sehemu hizi mbili ndipo Mwenyezi Mungu Huleta Nabii. Ambaye yeye huwarejesha katika njia iliyonyooka ili dunia iweze kwenda sawasawa. Watu wa Mungu huleta habari njema za kiroho. Lakini mambo hayo matatu yana uhusiano. Uzuri wa kiroho hapana shaka huwapelekea watu katika kutenda mambo mema na bila shaka matendo mema pia huleta maendeleo ya kimwili. Hata hivyo sio lazima kwamba mtu ambaye ana mafanikio ya kidunia awe ni mtu ambaye anafuata mambo ya kiroho au mtu mwenye tabia nzuri pia atakuwa mwenye maendeleo ya kiroho.

Mwenyezi Mungu Anataka kuwaleta wote hawa karibu na Yeye kwa hiyo Mwenyezi Mungu Ametayarisha mipango ya kuwaletea utakaso. Ili mafanikio ya kidunia yasiweze kuwa ni kizuizi katika kupata maendeleo ya kiroho. Mwenyezi Mungu Ameahidi ya kwamba Muaminio atapata ufaulu wa kila aina. Kuna njia nyingi za kupata ufaulu kitabia, kiroho na mafanikio ya kidunia. Lakini kuna njia ya ujumla ambayo ni kutengeneza uhusiano na Mwenyezi Mungu. Mafanikio yanapatikana kwa kujaribu kuipata njia hiyo, lakini matokeo ya jitihada hiyo yana mipaka yake. Hata hivyo wale ambao wanatafuta usafi wa nafsi hao wanapewa kila kitu. Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) hawakuchukua Baiat kwa sababu walikuwa wanataka mabarabara mapana au kuzunguukwa na usafi, isipokuwa wao walikiri kuwa "Hakuna Apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na Mtume Muhammad (saw) ni Mjumbe wa Allah", na hii ndiyo iliyotengeneza nafsi zao, lakini ni hii ndiyo iliyoleta ufaulu katika mambo yao ya kidunia.

Katika wakati wa Seyidna Umar (ra) Waislam walilazimika kuondoka Syria kwa ajili ya jeshi kubwa la Warumi. Wasyria walio Wakristo waliangua kilio, wakati Waislam walipoondoka. Na kwa hakika wakawakataza kuondoka, na wakasema tutakuwa na furaha mkiendelea kuwepo. Hao walikuwa Wakristo kama walivyokuwa Warumi. Lakini mfungamano wao na Waislam ulitokana na khulka njema na utawala mzuri wa Waislam. Ingawaje mambo ya utawala ni mambo ya kidunia Waislam wakati huo walipewa usafi wa nafsi.

Hadhrat Muslih Mauud (ra) anaeleza juu ya kisa cha mfanya biashara mmoja ambaye aliacha mali yake kwa Kadhi, aliporejea kutoka safari yake alikwenda kwa Kadhi ili kuomba amana yake, lakini Kadhi alikataa kata kata kwamba hakuwa na amana yake. Mfanyabiashara alipata simanzi kubwa na akajaribu kumueleza huku na huku begi hilo lilikuwa la aina gani n.k lakini hayo yote yalianguka katika sikio lililokufa. Katika sehemu hizo walikuwa na Mfalme ambaye ilikuwa ni rahisi kwenda kuonana nae. Mfanyabiashara huyo alifanya hivyo na akaenda kuzungumza na Mfalme juu ya mkasa mzima. Mfalme alitaka ushahidi wa yote hayo aliyokuwa anasema. Mfanyabiashara akasema hakuwa na ushahidi. Hivyo Mfalme akafanya mpango na mpango huo ulikuwa ni kwamba yule Mfanyabiashara akae karibu na Kadhi na yeye atakapokuwa anaingia basi yeye asimame na kuanza kuzungumza na Mfalme. Kwa hiyo akaanza kumpa maelezo. Na wakati huo Kadhi alimuona huyo Mfanyabiashara akizungumza na Mfalme kwa kitambo cha muda. Hapo yule Kadhi akahisi kwamba huenda habari yote ya ule mkoba wa amana imeelezwa kwa Mfalme, kibinadamu ni lazima alihofia kupata chamtemakuni, mara tu yule alipomaliza kuzungumza na Mfalme alimwita kando na kumueleza kuwa; bwana wangu kuhusu ule mkoba ni kweli!, unajua tena umri wangu umekuwa mkubwa, hivyo kiasi fulani ninasahau kwa urahisi, lakini nakumbuka kuhusu ule mkoba. Na hivyo baadae akauleta ule mkoba na kumkabidhi amana yake. Jambo la kuzingatia ni kwamba ni kuwa kama urafiki na mfalme tu wa kidunia unapata faida kiasi hicho, je ukijenga urafiki na Allah itakuwa faida kiasi gani?

Lakini imani inahitajika kwa ajili ya hili, imani inayovutia radhi za Mwenyezi Mungu. Mtu mwenye imani ya kweli hawezi kamwe kutupilia mbali tabia njema. Iwapo atashikilia tabia zote njema na kuzitekeleza atafikia kuwa mkweli, mwaminifu, mwenye kuchunga amana, mchamungu na msafi. Na jambo hili litampelekea yeye kupata elimu, amali, uhodari, utambuzi, uwezo na umakini na sifa hizo zitampelekea pia kupata mafanikio ya kidunia. Mwaminio wa kweli anatakiwa daima awekeze zaidi kwenye maungano ya kiroho. Mwanadamu huwa hazawadiwi hadi pale anapofikia kilele juu ya jambo fulani, na hivi pia ndivyo ilivyo kwenye dini na hivyo mtu anatakiwa ajitahidi kufikia kilele.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akisema watu wanaofaidika nami ni wale tu walio na maungano makubwa na mimi, au wale wanaonipinga sana, kama vile Maulawi Sana Ullah Sahib na wale wengine ambao wanajulikana makhsusi kwa sababu ya kumpinga yeye au wale walio na mafungamano ya kweli naye. Mahusiano ya juu juu tu hayana manufaa. Iwapo mtu atamwelekea Mwenyezi Mungu atatendewa jinsi walivyotendewa wale wa mwanzo. Iwapo mtu atajitahidi sana kwa hili atalifikia. Kinachohitajika ni kujitupa kwa Mwenyezi Mungu kwa uaminifu na ikhlas ya kweli na jambo hili ndilo liletalo mafanikio.

Tufanye juhudi kumfikia ukaribu na Mungu, tujitahidi kupata uelewa wa dini iliyoshushwa na Mungu na tujitahidi kuyafanya Mapenzi ya Mungu kuwa sehemu muhimu ya maisha yetu. Jambo hili litatupelekea kuwa na khulka njema na hatimae kukua kwenye maendeleo ya kidunia pia. Iwapo tutajitahidi kujichotea mwanga wa kiungu kwa hakika tutapata baraka za Mwenyezi Mungu. Iwapo tutajitahidi kujichotea mwanga wa kiungu kwa moyo wote utaifukuzilia mbali kiza cha uongo, udhaifu, na ulaghai pamoja na magonjwa mengine na khulka njema za kiwango cha juu zitazalika ndani yetu. Iwapo tunapenda kukiokoa kizazi chetu kijacho kutokana na athari mbaya ya kidunia kuna haja ya lazima ya kuwafafanulia maungano yaliyopo baina ya dini na tabia njema. Iwapo tunapenda kupata ufaulu wa kidunia ukiungana na maendeleo ya kidini na ya kiroho kuna ulazima wa kujitahidi kuungana na Mwenyezi Mungu sisi wenyewe binafsi.

Amin.

Waahmadiyya na Mwalimu Nyerere

Kutoka uk. 12

waige mwenendo wa Jumanne Rashidi Abdallah. Mwalimu Nyerere aliwaambia vijana kuwa siku zote Jumanne Rashidi Abdallah anapotumwa kufanya kazi za chama haombi hata senti tano, na anajitolea sana. Mwenendo huu ulimvutia sana Mwalimu Nyerere na akataka vijana wamuige Bw. Jumanne.

Tabia nyingine iliyomvutia sana Mwalimu na akawa karibu na kijana huyu (Jumanne Rashidi Abdallah) ilikuwa ni ile tabia ya kutokuwa 'ndio Bwana' kukubali bila kujengewa hoja ilimuradi kumfurahisha kiongozi. Mwenendo huo hakuwa nao.

Kwa mfano kwenye mkutano nyeti wa Tabora wa chama cha TANU juu ya kushiriki au kutoshiriki katika kura tatu, Bw. Jumanne Rashidi Abdallah alitofautiana vikali sana na Mwalimu Nyerere. Yeye Jumanne Abdallah alipiga kura ya kupinga masuala ya mseto, alisimama akajenga hoja bila ya kupayuka au kupiga kelele. Tabia hiyo ya kutoa maoni yake bila woga isipokuwa kwa hoja hivyo vyote vilimvutia sana Mwalimu Nyerere. Na hata kama tofauti hizo zilijitokeza Mwalimu aliendelea kufanya kazi na Bw. Jumanne Abdallah na ushahidi ni huo alipochaguliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga pindi tulipopata uhuru.

Mwalimu Julius K. Nyerere alikipenda sana Kiswahili na ushahidi wa kutosha upo. Mara kwa mara aliwaita washairi Ikulu na kubadilishana nao mawazo. Aliwapatia Ofisi ya kudumu katika jumba la Anatoglo, alihudhuria mchezo wa kuigiza wa Julius Kaisari alioutafsiri yeye mwenyewe kutoka katika Kiingereza kuja kwenye Lugha ya Kiswahili huko shule ya Pugu, alimuomba Pal Sozigwa atafsiri shairi 'Song of Lawino' katika Kiswahili na alihudhuria uzinduzi wa utenzi mrefu katika Kiswahili '*Rasil ghuli*' na alitoa jina la shule ya Shaaban Robert kwa kumbukumbu ya mshairi maarufu wa mashairi ya Kiswahili.

Ndio maana rafiki zake waliomzunguuka siku hizo za mwanzo za mapambano ya uhuru walikuwa ni wapenzi wa Kiswahili. Akina Saadan Abdul Kandoro, Shaaban Gonga, Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jumanne Rashidi Abdallah. Jumanne Rashidi Abdallah alikuwa ni bingwa wa Kiswahili na ushahidi ni kushiriki kwake katika kile kipindi maarufu cha "*Mbinu za Kiswahili*" kilichokuwa kinaongozwa na Suleiman Hega wakiwemo pia wataalamu wa Kiswahili akina Abdullatifu Abdallah, Abdul Bari Diwani, Mathias Mnyampala, Mohammed Alli na Jumanne Rashidi Abdallah. Mapenzi na ubingwa wa Jumanne Rashidi Abdallah katika Kiswahili ulijidhihirisha katika kipindi hicho. Na inasimuliwa ya kwamba ilikuwa muhali kwa Mwalimu Julius K. Nyerere kukikosa kipindi hicho. Na pindi alipopata nafasi pia aliweza kufanya masahihisho katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mathalani alikemea sana neno 'Masaa' akisema ya kwamba hakuna neno 'masaa' katika Kiswahili. Wingi ni ule ule 'saa'.

Kwa ujumla Mwalimu Nyerere alikuwa karibu sana na Jumanne Abdallah kwa sababu ya mapenzi yao wote wawili kwa lugha hii adhimu Kiswahili ambayo inachukua nafasi yake adhimu katika lugha maarufu barani Afrika.

Maungano na Mwenyezi Mungu ndio Msingi wa maendeleo yote

Kutoka uk. 12

Swali linaloulizwa leo sio geni; hili limekuwa likiulizwa hata huko nyuma kwa sababu watu wengi hawajitahidi kuelewa maana ya kweli ya dini. Wale wajiitao wanaulamaa wa kidini wanaiwakilisha kwenye sura ya uzushi, wanatoa majibu yenye makosa kwa watu na hivyo kuwaingiza wasomi (wa elimu ya kidunia) kwenye mkanganyiko zaidi. Wakati mwingine watu wenyewe wanafanya maamuzi na kutoa majibu yasiyo sahihi juu ya dini.

Mwenyezi Mungu Alimtuma Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili kukabiliana na matatizo haya na kuyapatia ufumbuzi, naye ametupatia hayo. Hadhrat Musleh Mauud r.a. alitoa hotuba ya Ijumaa ambamo ndani yake alionyesha muunganiko au mahusiano yaliyopo kati ya tabia njema, maendeleo ya kidunia na dini na Uislamu unaliangaliaje jambo hilo na ni kwa namna gani Mtume Muhammad s.a.w. alilionesha kwenye matendo yake ya kila siku.

Akasema: Ni jambo gumu kuvitenganisha dini, tabia njema na maendeleo ya kidunia ya mwanadamu. Mtu anayeshika dini hawezi kuzitengenisha tabia njema na dini lakini pia hawezi kuliacha wazo la kupata mahitaji yake ya kidunia. Kwa hakika kama iwe hivyo basi maendeleo yote ya kidunia yatasita. Hata hivyo ingawaje mambo hayo yameshikana, lakini bado yanaachana na inabidi yatenganishwe. Watu wasiofuata dini wanashikilia kwamba mtu anahitaji kuwa na tabia njema na maendeleo ya kidunia. Ingawaje Muislamu wa kweli anashikilia kwamba mwanadamu pia anaihitaji dini kwa sababu dini inambeba mtu kumfikisha kwa Mungu.

Islam pekee ndio dini inayounganisha kwa pamoja maendeleo ya kiroho, tabia njema na maendeleo ya kidunia. Ingawaje waislamu walio wengi hawatambui ukweli wa dini yao na jinsi inavyoungana na tabia njema na maendeleo ya kidunia badala yake wanakuwa wenye mihemuko ya kidini iliyopita kiasi (iliyochupa mipaka) kiasi hiki kwamba wanawafanya watu wawe mbali zaidi na dini. Mbali na ibada za msingi za Islam kama vile sala na saumu, baadhi ya wanaulama wa kiislam wanasisitiza juu ya mambo kama vile makongamano na maandamano kwamba nayo ni sehemu ya dini na kwamba wale wasioshiriki kwenye hayo basi si waaminio au wameritadi. Na kwenye hili pia wanaulamaa wanapishana mawazo na kila kundi linatoa fatwa dhidi ya kundi jingine na hapo hitilafu zinazidi kuongezeka.

Haya yote hupelekea kwenye makundi yenye misimamo iliyochupa mipaka kutengeneza kile wakiitacho sharia za kidini na hapo kupelekea kwenye mauaji na maangamizi ya wanadamu. Hali ilivyo huko Syria, Iraq, Afghanistan na Pakistan inatokana na sheria za kubuni ambazo zimetengenezwa kwa jina la dini!

Mwandishi mmoja wa Kifaransa ambaye ameachiwa karibuni na kundi la ISIL anasema aliona mambo kadhaa yakifanywa kinyume kabisa na uelewa wa Islam alionao. Alipowauliza baadhi ya watu kwenye kundi hilo la ISIL kuhusu hayo walimwambia kwamba wao hawaelewi aya wala hadithi inayofundisha hayo wayafanyayo bali wakifanyacho ni sheria waliojiwekea wenyewe.
Hali inayoendelea huko Yemen pia nayo ni dhirisho la utekelezaji wa sharia zinazowekwa kulipendelea kundi fulani kwa jina la dini, na hivyo kupelekea kuwauwa watu wasio na hatia kwa makombora. Bila shaka ni kweli kwamba makundi yote hayako sahihi lakini hilo halihalalishi pia kwamba kundi moja liwauwe wengine. Kila kiongozi wa dini na kila 'maulana' anaonekana amejitengenezea dini yake mwenyewe na kamwe hakuna uhusiano kati ya Uislamu wa kweli na uislamu huo wautekelezao wao. Hii ndio moja ya sababu kubwa kwamba watu wengi wameachana kabisa na dini.
Kwa upande mwingine wale wajiitao wasomi wa Kimagharibi wasioamini dini wanajaribu kuvitenganisha tabia njema, maendeleo ya kiroho na maendeleo ya kidunia na kuonesha kwamba si vitu vinavyokwenda pamoja. Iwapo wanatafakari juu ya jambo liitwalo 'Wahyi' wao husema kwamba hilo ni hisia tu za kibinadamu na wanashikilia kwamba ni tabia njema tu ndizo ziifaazo dunia. Wanatafakari juu ya dini na kusema kwamba dini wakati fulani ilihitajika na iliwasaidia watu ambao hawakuwa wameelimika au walikuwa na elimu ndogo ili wasitende maovu, na wanasema kwamba kwa leo ambapo watu wameelimika vya kutosha na tayari wanazo tabia njema hakuna tena haja ya dini.

Tunapotafakari juu ya tabia njema, maendeleo ya kiroho na maendeleo ya kidunia tunaona kwamba mambo hayo yamevaana kiasi hiki kwamba si kila mtu anaweza kuyaona ni vipi yameshikana. Tunapoangalia maisha yaliyobarikiwa ya Mtume Muhammad s.a.w. ndipo tunapoelewa mahusiano hayo. Mtume Muhammad s.a.w. alikuwa ni mhuishaji mkuu wa dunia wa mambo ya kiroho, tabia njema na maendeleo ya kidunia pia. Maisha yake yaliyobarikiwa ni dhihirisho la hayo yote kwa pamoja. Alisema bila ya sala na maombi imani ya mtu haiwezi kukamilika. Kwa maana kwamba wakati kumuabudu Mungu ni jambo la lazima lakini alisisitiza pia maendeleo ya kiroho. Akaonyesha kwamba mahusiano baina ya sala (maombi) na mwanadamu ni kama yalivyo mahusiano baina ya mama na mtoto.

Dua maana yake ni kumuita fulani na mtu huweza tu kumwita mwingine pale anapokuwa na uhakika kwamba huyo anayemwita atakuja kumsaidia. Mambo matatu ni ya lazima ili mtu aweze kumwita mwingine kwa ajili ya msaada. Kwanza ni lazima mtu awe na yakini kwamba wito wake utasikika. Pili mtu lazima awe na yakini kwamba huyo anayemwita anao uwezo wa kumsaidia; na tatu mtu ni lazima awe na mapenzi ya asili na utii kwa huyo anayemwita kwa ajili ya msaada na pia ni lazima aelekee kwake tu na si kwa mwingine yeyote.

Mambo mawili ya kwanza yanahusiana zaidi na akili. Iwapo mtu hana uhakika kwamba sauti yake itasikika na iwapo pia hana uhakika kwamba huyo anayemwita anao uwezo wa kumsaidia bila shaka litakuwa ni jambo la uwendawazimu kumwita huyo kwa msaada. Jambo la tatu ingawaje linahusiana na asili ya mwanadamu. Ni mapenzi ya asili na utii ndio yanayomfanya mtu asikielekee chochote kingine zaidi ya kile akipendacho.

Ni kama yalivyo mapenzi ya asili kati ya mama na mtoto. Hata kama mtoto anayezama kwenye maji anaelewa kwamba mama yake hawezi kuogelea, iwapo yupo karibu ni huyo mama ndiye mtoto atamwita aje kumsaidia na si mwingine yeyote. Hii inatokana na mahusiano ya hisia za ndani ambayo Mtume Muhammad s.a.w. alisema imani haiwezi kukamilika bila ya maombi. Aliyaangalia mahusiano kati ya Mungu na mja wake kuwa ni kama mahusiano ya mama na mtoto ambapo mtoto katika hali yoyote anamkimbilia mama kwa msaada.

Jambo la pili ni tabia njema. Tunaona mifano ya kila hali na kila aina katika maisha yaliyobarikiwa ya Mtume Muhammad s.a.w.. Tunaona mfano wake mwema wa jinsi alivyoonesha mapenzi kwa wake zake hata katika mambo madogo sana jambo ambalo ni la muhimu sana kwa maisha ya furaha kwenye familia. Mapenzi yake na hadhari yake kwa wake zake yalikuwa kiasi hiki kwamba kama mke wake alikunywa maji kwenye kikombe basi naye angeangalia mahala pale pale aliponywia mke wake ili naye anywe. Kwa sura ya nje jambo hili linaweza kuonekana dogo lakini linaonyesha hali ya ndani ya mapenzi yake.

Hii inaonesha kwamba mapenzi sio kuonesha mambo makubwa tu bali yanajionesha zaidi kwenye mambo madogo madogo. Maisha yaliyobarikiwa ya Mtume Muhammad s.a.w. yana mifano lukuki inayoonesha tabia zake njema za kushangaza kabisa kiasi hiki kwamba maisha yake yote yanaonekana alikuja kusoma na kufundisha tabia njema. Alikuwa ni mfano wa pekee katika kujali mafungamano ya ubinadamu, mafungamano ya kindugu, kupiga vita uongo, ulaghai na utovu wa amana.

Jambo la tatu ni hili kwamba mafundisho yake yaliongoza pia kwenye maendeleo ya kidunia. Kwa mfano aliwasisitiza watu juu ya umuhimu wa kuziweka barabara kuwa wazi kwa ajili ya maisha ya jamii, juu ya upatikanaji wa maji safi, usafi wa barabara, na pia alitoa ushauri juu ya kuzifanya nyumba kuwa na hewa safi. Pia aliwasisitiza wafuasi wake wajali mambo ya kidunia kwenye uongozi, utamaduni, viwanda na biashara. Hata hivyo kinyume na wale waitwao maulamaa wa kidini leo, Mtume Muhammad s.a.w. hakulielewa kila jambo kuwa ni lazima lichukuliwe kuwa ni la kidini.

Kwa mfano, Siku moja Mtume Muhammad s.a.w. aliwoana watu wakibebesha mitende kwa kuchukua maua ya masuke dume na kuyakung'utia kwenye maua ya kike. Akawauliza kwa nini wanahangaika hivyo, wasiwachie hali hiyo kutokea kwa njia ya kawaida tu ya upepo? Wakulima wale wakawacha kubebesha, lakini ikatokea kwamba mwaka huo mavuno yakawa machache sana. Wakati Mtume Muhammad s.a.w. alipofahamishwa juu ya sababu ya kupata mavuno machache kwamba ni kule kuacha kubebesha maua, aliwaambia kwamba yeye hakuwaamuru wasibebeshe maua. Akasema elimu yao kwenye utaalamu huo wa kilimo ilikuwa ni kubwa kuliko yeye. Na hapa Mtume Muhammad s.a.w. akatuonesha jinsi alivyotengenisha mambo ya kidunia na yale ya kidini.

Hapa tunao mfano wa Mtume Muhammad s.a.w. ambao akiwaambia watu kwamba wao wanaelewa zaidi juu ya mambo yao ya kidunia kuliko yeye lakini tunao Maulawi (masheikh) wa leo ambao wako tayari saa yoyote kumtangaza mtu kwamba ameutoka uislamu (ameritadi) kama kuvua kofia vile. Na kwa upande mwingine kuna upande wa shilingi wa mafilosofa wa kimagharibi ambao wao wanasisitiza na kusisitiza juu ya maendeleo ya kidunia tu.

Mafilosofa wao wanasema sio swali la Mungu kumuumba mtu bali (*naudhu Billaahi min dhaalika*) ni jinsi mtu alivyomuumba Mungu kwenye mawazo yake. Wanadhani kwamba watu waliendelea kutafuta mfano mzuri wa kuiga na kwa kukosa mfano huo kwa muda mrefu mawazo yao yakaenda mbali kwenye kitu kilichokamilika na hatimae kikaitwa Mungu. Hivi ndivyo ambavyo watu hawa wanadhani juu ya wazo la kuwepo kwa Mungu na maendeleo ya kidunia. Kidogo kidogo wameachana na dini na mafilosofa wao wa leo nao wamegeukia kuwa 'madahari' wasioamini kuwepo kwa Mungu. Watu wengi sana katika ulimwengu wa kimagharibi hawaamini kuwepo kwa Mungu nao hudhani kwamba kuwa na tabia za utu na maendelo ya kidunia ndio kila kitu. Na kwa upande mwingine Maulawi wa leo nao ni wachokozi mno na wanakihesabu kila kitu kuwa ni cha kidini. (wanakijua zaidi wao watu wa dini).

Tunayo bahati kubwa sisi Waahmadiyya kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametuokoa kutokana na mikanganyiko hiyo na ametuongoza kwenye kushika mwenendo uliobarikiwa wa Mtume Muhammad s.a.w. ambaye alifundisha njia ya kati kati (wastani) katika kila kitu. Alifundisha kwamba bila shaka yoyote kumuabudu Mungu ni jambo muhimu kabisa, bali ndio lengo la maisha ya mwanadamu, lakini pia nafsi ya mtu mwenyewe nayo inayo haki zake kama vile ambavyo mke wake, watoto wake na majirani zake nao wanazo haki zao. Ili kutimiza haki hizi ni lazima tutumie njia 3. Kwanza

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jumd.2 - Sha'ban 1436 AH | April/May 2015 | Shah./Hijr. 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir bin Abdillah r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Msijifunze elimu kwa nia ya kuona fahari mbele ya wataalamu wengine wala kwa kuringa mbele ya wasio na ujuzi na kuwagombanisha, wala msifanye vikao kwa kuonesha elimu yenu. Atakayefanya hayo atapata moto! Naam moto! (*Ubn Majah*).

Maungano na Mwenyezi Mungu ndio Msingi wa maendeleo yote - Khalifa mtukufu

Na mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani, Hadhrat Khalifa tul Masih wa Tano ayyadahullahu taala binasrihil Aziz (a.t.b.a.) alitoa hotuba ya Ijumaa tarehe 24 Aprili, 2015 katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London nchini Uingireza. Katika hotuba yake baada ya kusoma tashahhud na sura Al-faatiha, Huzur alisema kuwa:

Swali ambalo linaulizwa sana siku hizi na pengine linaulizwa zaidi kuliko zamani na vijana, wale ambao hawakupata mwongozo sahihi na wale ambao hawafuati dini kabisa, ni kwamba kwa vile elimu ya kidunia inaweza kumfanya mtu kuwa na tabia njema, sasa kuna haja gani ya kufuata dini? Inasemwa kwamba tabia njema zinaweza kufikiwa bila ya elimu ya dini, na kwa kweli watu hawa wanashikilia kwamba duniani leo watu wasiofuata dini wanaonekana kuwa na tabia bora zadi kuliko wale wanaofuata dini. Makhsusi hoja hii inaletwa dhidi ya wafuasi wa dini tukufu ya Islam. Kwa sababu watu wa dini zingine kiujumla wameshajiweka mbali kabisa na imani zao lakini kwa upande wa waislamu hata wale wasiotekeleza chochote katika dini yao bado wanajinasibisha na imani yao waliyozaliwa nayo, basi kwa hakika pingamizi hii inaletwa dhidi ya waislamu.

Jitihada zinafanywa kuwashawishi vijana kuachana na dini. Sehemu kubwa ya elimu ya kimagharibi inasisitiza kwamba mtu afanye uchunguzi na ugunduzi kwa kutumia vitu vinavyoshikika. Wazazi wengi hawawajibu watoto maswali haya ipasavyo wanapowauliza juu ya mambo haya, ama kwa sababu ya kukosa muda kutokana na majukumu ya kijamii waliyonayo yatokanayo na mbinyo wa kiuchumi, au kwa sababu hawana elimu kabisa.

Mara kadhaa badala ya kuwajibu vijana wao wazazi wanayakandamiza mawazo yao. Hili huwafanya vijana waone kwamba ingawaje Islam inajitaja kuwa ni dini ya kweli na inayo majibu ya matatizo yote, lakini inaonekana haina majibu yanayoshikika na kutekelezeka na yanayokwenda na wakati.

Bila shaka Islam ndio dini iliyokamilika na Qurani tukufu ndicho kitabu kikamilifu na mwenendo uliobarikiwa wa Mtume Muhammad s.a.w. ambao ndio picha ya Qur'an tukufu uko mbele yetu. Ni mwenendo wake uliobarikiwa ndio uliozalisha mabadiliko ya kimapinduzi kwenye maisha ya masahaba zake r.a., waliielewa imani, wakafahamu maana ya tabia njema, na pia wakapata maendeleo makubwa ya kidunia. Wakakiweka kila kimoja katika hivyo vitatu mahala pake pafaapo.

Vijana wajaribu, bali kwa hakika wakubwa pia wafanye hivyo, kuelewa maana ya kweli ya tabia njema, maendeleo ya kidunia na maendeleo ya kiroho na kisha wakiweke kila kimoja mahala pake. Iwapo vijana watalielewa jambo hili litafungua kwao milango yote ya maendeleo na watapata kuelewa ni uzuri kiasi gani uliomo kwenye mafundisho ya Islam na pia watapata kutambua uongo uliomo kwenye hoja za wale waupingao.

Endelea uk. 11

Waahmadiyya na Mwalimu Julius Nyerere

Na Mahmood Hamsin Mubiru,
Dar es Salaam

Ukitizama picha ya kuapishwa kwa wakuu wa mikoa wa mwanzoni tulipopata uhuru utagundua kuwa asilimia 10 ya wakuu hao walikuwa ni Waahmadiyya. Wakuu hao ni pamoja na Sheikh Kaluta Amri Abedi aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora mahala alipofanya kazi na kudharauliwa sana na kusaidiana na Sheikh Mubaraka Ahmad katika kazi ya kuhubiri dini tukufu ya Islam na kuifanya kazi ile adhimu ya kumsaidia katika kutafsiri Qur'an Tukufu katika lugha ya Kiswahili. Na mwingine alikuwa kiongozi wa mstari wa mbele wa viongozi wa vijana msomi wa shule ya Tabora fundi wa ujengaji hoja bila woga Bw. Jumanne Rashidi Abdallah aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga. Sehemu iliyokuwa na upinzani mkubwa dhidi ya jumuiyya ya Ahmadiyya.

Mwalimu Nyerere katika msikiti wa Ahmadiyya Dar es Salaam.

Bw. Jumanne Rashidi Abdallah alijiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya akiwa bado yupo shuleni Tabora, huko alikutana na masheikh wa Kiahmadiyya na kutokana na kukubaliwa kwa maombi yaliyofanywa na wao Bw. Jumanne Rashidi Abdallah aliweza kupona na hatimae aliweza kujiunga na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya.

Vitabu vingi vilivyotolewa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya na gazeti la Mapenzi ya Mungu vilimfanya atambue ya kwamba uhuru halikuwa jambo la ihsani, bali ilikuwa ni suala zima la haki ya binadamu. Ulimvutia sana utangulizi ulioandikwa na Hadhrat Mirza Bashirudin Mahmood Ahmad Khalifa wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa (as) katika tafsiri ya kwanza ya Qur'an Tukufu katika Kiswahili. Katika tafsiri hiyo Khalifa Mtukufu anawaita Waafrika waifuate Qur'an Tukufu ili wapate uhuru wa kweli na watoke katika minyororo ya ubeberu.

Hivyo basi alipojiunga na chama cha TANU mwaka mmoja baada ya chama hicho kuzaliwa yaani 1955 aliingia na msimamo na uhakika ya kwamba jambo lililokuwa linapiganiwa na TANU lilikuwa ni la haki na wala sio uasi. Mambo mengi aliyoyakuta katika Jumuiyya ya Ahmadiyya kama ya kutii viongozi, kuheshimu mamlaka na mfumo vilimfanya alipoingia katika chama cha TANU aweze kung'ara na kufanya kazi iliyosifiwa na viongozi wa chama hicho cha ukombozi.

Kwa mfano katika Jumuiyya ya Ahmadiyya upo utamaduni wa kujitolea kwa hali na mali ni jambo la kawaida kufanya kazi bila malipo na upo utamu wa ajabu katika kujitolea. Utamaduni huu uliwashangaza na kuwaathiri vijana wengi katika umoja wa vijana.

Mwalimu Julius K. Nyerere alifikia hatua ya kuwaambia vijana wa chama cha TANU

Endelea uk. 10